

USHINDI WA ISLAM

NA

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s.

Mfasiri
Sheikh Bakri Abedi Kaluta

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

USHINDI WA ISLAM
Swahili translation of Fat'he Islam

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1891
Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2009
Nakala: 2500

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mnazimmoja, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031
ISBN: 9987-438-04-0

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
تَحْمِدُهُ وَتُنَصِّلُهُ عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ^١

MAELEZO YA MWENEZI

Naona furaha kuweka mbele ya wasomaji tafsiri hii ya kitabu cha Seyyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kitiwacho ‘*Fat’he Islam*’, **Ushindi wa Islam**. Kitabu hicho kiliandikwa mnamo mwaka 1890 na kilichapishwa mwanzoni mwa mwaka 1891.

Katika kitabu hicho Seyyidna Ahmad a.s. ameeleza matawi matano ya kupata ushindi wa Islamu na akatangaza kwamba:

“Masihi Aliyetabiriwa kuja ndiye huyu, mkitaka mkubalini. Mwenye masikio na asikie.” uk.9

“Nimetumwa kwa jina la Masihi ili itikadi ya msalaba ivunjiliwe mbali. Hivyo, mimi nimetumwa kwa kuvunja msalaba na kuua nguruwe. Nimeshuka toka mbinguni pamoja na Malaika Watakatifu waliokuwa kulia na kushoto kwangu.” uk. 10

“Enyi Waislamu, kudhihiri kwangu kwa kuondoa magiza ya kiuchawi ni mwujiza kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

¹ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Mtukufu.

Je, haikulazimu kwa kupambana na uchawi, mwujiza pia ungekuja duniani” uk.5

Yafaa nieleze kwamba mnamo mwaka 2005, Hadhrat Khalifatul Masihi V (a.t.b.a) alipotembelea Afrika Mashariki alisikia sana haja ya vitabu vya Seyyidna Ahmad a.s. kufasiriwa kwa Kiswahili. Akatoa amri ya kuteua jopo maalum nchini Tanzania kwa kushughulikia kazi hii muhimu ya kufasiri. Akaagiza pia kuanzisha ‘*Deski ya Kiswahili*’ hapa katika Wakalate Tasnif, Rabwah, Pakistan. Kitabu hiki, ‘*Ushindi wa Islamu*’, ni tunda la mpango huo aliofanya Khalifa wetu Mtukufu.

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta wa Tanzania na kusahihishwa na wataalamu wa Kiswahili Bwana Mahmudu Hamsini Mubiru na Bi. Radhia Kaluta wa Tanzania.

Hapa Makao Makuu katika ‘*Deski ya Kiswahili*’ Sheikh Jamil R. Rafiq na Sheikh Bashir A. Akhtar wakaichunguza tafsiri hii na kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu. Lakini katikati ya shuguli hii, Sheikh Bashir A. Akhtar akatuacha mkono. Sisi ni wa Mungu, na Kwake tutarejea. Mungu Amweke pema Peponi. Mahali pake Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri wa zamani katika Kenya, Tanzania na Ghana, na baadaye Sheikh Mubarak Mahmud ambaye aliwhi kukaa Tanzania, wakaungana na ‘*Deski ya Kiswahili*. ’

Aidha ndugu kadha wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal, Bwana Farrukh Javed na Sharifu Tanwir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad ‘Ali
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid
Rabwah, Pakistan
23 March, 2008

TANGAZO

Katabu hiki ‘Fat’he Islam’(Ushindi wa Islam) kimechapishwa nakala mia saba. Mia tatu kati ya hizo zimetolewa wakfu, kwa kutafuta radhi ya Mungu tu kwa ajili ya wahadhiri wa Kiislamu au kwa wenyе hali ndogo walio na shauku au kwa wanazuoni wa Kikristo au wa Kibanian. Nakala mia nne zilizosalia ni kwa wale walio na uwezo wa kununua, kwa bei ya anna nane (senti hamsini) kwa nakala moja, mbali na gharama ya posta. Mionganoni mwa wahadhiri au wenyе hali ndogo, anayetaka kupata bure anapaswa kuleta stempu ya nusu anna (senti mbili) tu na kitabu kitatumwa.

MTANGAZAJI
Mnyenyeketu
Mirza Ghulam Ahmad
(Mungu Amsamehe)
Wa Qadian

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ²

نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ³

USHINDI WA ISLAM NA HABARI NJEMA KUHUSU ONYESHO MAALUM LA MWENYEZI MUNGU NA WITO KWENYE NJIA ZA KUMFUATA NA NAMNA ZA KUPATA MSAADAA WAKE.

رَبِّ افْتَحْ رُوحَ بَرَكَةً فِي كَلَامِنِ هَذَا وَاجْعَلْ أَفْئِدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوَى إِلَيْهِ⁴

Enyi wasomaji, Mwenyezi Mungu Awajaalieni heri katika dunia na dini. Leo baada ya muda mrefu ninawaelekezeni kwenye madhumuni muhimu yahusikanayo na mpango wa Mwenyezi Mungu Alionikabidhi kwa kuihami dini ya Kiislamu. Nami katika madhumuni haya, kadiri Mwenyezi Mungu Alivyonijaalia kutoka Kwake kipawa cha kueleza bayana, nataka kuwadhihirishieni adhama ya Jumuiya hii na haja ya kuusaidia mpango huu, ili nipate kutimiza wajibu wangu wa kufikisha ujumbe ipasavyo. Hivyo, katika kuyabainisha madhumuni haya mimi sijalikwamba maandishi haya yataathirije mioyo. Shabaha ndiyo tu kwamba jambo ninalowajibikiwa na ujumbe ambao kuufikisha ni kama

² Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

³ Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Wake Mtukufu.

⁴ Ee Mola wangu, pulizia roho ya baraka ndani ya maneno yangu haya na ujaalie mioyo ya watu ilekee kwayo.

deni la lazima kwangu niutekeleze ipasavyo, ijapokuwa watu wasikilize kwa furaha au waone kwa kuchukia au kutokupenda ama wadhanie vema au vibaya.

وَأَفْوَضْ أَمْرِنِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ بِحِسْبَرٍ بِالْعِبَادِ⁵

Sasa naandika hapa chini madhumuni niliyoyaahidi juu.

Enyi watafutao ukweli na wapenzi wa kweli wa Islam, ni wazi kwenu kwamba zama hizi tunamoishi ni zama za giza ambamo mambo yote, yawe ya kiimani au ya kima-tendo, yamechafuka sana na upepo mkali wa upotetu unavuma kutoka kila upande. Kitu kinachoitwa imani, kimekuwa ndiyo maneno matupu yanayotamkwa tu kwa ulimi. Na mila chache au ubadhirifu na shughuli za kujionyesha zimefahamika kuwa ndiyo mambo yanayoitwa matendo mema; na wema wa kweli hawana habari nao kabisa. Falsafa na sayansi ya zama hizi pia yapinzana vikali na nguvu za kiroho. Mvutano wake huwaathiri vibaya sana wanayoilewa na kuwasukuma kwenye giza. Huo unachochea sumu ya maovu na kumwamsha Shetani aliylala. Wajuao elimu hizo mara nyingi huwa na imani mbovu kuhusu mambo ya kidini hata kwamba hudharau na kudhihaki sheria zilizowekwa na Mwenyezi Mungu na njia za ibada za saumu na sala na kadhalika. Miayoni mwao hamna heshima yoyote wala taadhima ya Mwenyezi Mungu, bali wengi wao wanamkana

⁵

Nami ninamkabidhi Mwenyezi Mungu jambo langu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Awaonaye watu.

Mwenyezi Mungu na wamejaa udaharia na wakijiita wazao wa Waislamu ndio maadui wa dini. Wale wasomao vyuoni mara nyingi, hutokea hivi kwamba kabla hawajahitimu masomo ya lazima huwa wamekwisha ondokewa dini na huruma yake. Hili ni tawi moja tu nililotaja ambalo katika zama hizi limejaa matunda ya upotevu. Lakini zaidi yake kuna mamia ya matawi mengine pia yakiwa na hali hiyo. Huonekana kwamba amana na uaminifu umeondoka duniani kana kwamba umetoweka kabisa. Kwa kujichumia dunia hila na udanganyifu vimepitaki. Yule aliye mkorofsi zaidi ndiye anahesabiwa hodari zaidi. Aina mbalimbali za uwongo, hiana, uasherati, udanganyifu, ulaghai, uchuku, ujanja wa hali ya juu na hila zenye tamaa tupu na tabia zilizojaa maovu huendelea kutapakaa. Na chuki na magomvi yasiyo na huruma yanaendelea kuzidi na tufani ya tabia za kinyama na kimbuai imevuma. Na kadiri watu wanavyokuwa hodari katika elimu na kanuni hiso, ndivyo wanavyopungukiwa tabia za asili za wema na mwendo mwema na sifa za asili za kuona haya na ucha-Mungu na uaminifu.

Mafundisho ya Wakristo pia yanatayarisha mashimo mbalimbali yabarutikulipua ukwelina uaminifu. Na Wakristo, kwa kufutilia mbali Islam, wakizusha njia zote za kisiri za uwongo na uzushi, kwa juhudhi kubwa kabisa wanazitumia kwa kunyanganya, na mbinu mpya mpya za kudanganya na njia mpya za kupoteza zinaundwa. Na wanamfedhehesha mtu mkamilifu aliye fahari ya watakatifu wote na taji la watawa

wote na mwongozi wa Mitume wote watukufu hata kwamba katika drama sura za Islam na mwongozi mtakatifu wa Islam zinaonyeshwa kwa njia mbaya na michezo ya kuigiza huonyeshwa na tuhuma za kiuzushi zinaenezwa kwa njia ya majumba ya michezo ambamo ushenzi wote umetumiwa kwa kufedhehesha Islam na Nabii Mtukufu s.a.w.

Sasa, enyi Waislamu, sikilizeni, tena sikilizeni kwa makini kwamba kwa kuzuia athari takatifu za Islam, uzushi wenye udanganyifu ultumiwa sana na taifa la Kikristo na hila zenye ulaghai zilitumika, na ili kuzieneza hizo, juhudhi nyingi zilifanywa kwa kutumia mali nyingi ajabu bila kujali hata kwamba njia zote zenye aibu ambazo afadhali zisiezwe katika madhumuni haya, zimemalizwa kwa shabaha hiyo. Hizo ndizo harakati za udanganyifu za mataifa ya Kikristo na wenye kuamini Utatu. Kwa kupambana na udanganyifu wao huo, Mwenyezi Mungu Asipoonyesha mkono wenye nguvu ambao una uwezo wa kimwujiza, na kwa mwujiza huu Asipofutilia mbali udanganyifu huo, watu wa kawaida kusalimika katika mizungu hiyo ya Wazungu, ni jambo lisiloweza kuwazwa na kufikiriwa. Hivyo, kwa kubatilisha “uchawi” huo, Mwenyezi Mungu Amewapa Waislamu wa kweli wa zama hizi mwujiza huu kwamba Yeye Amemtuma mtumishi Wake huyu kukabiliana na wapinzani kwa kumjaalia ufunuo Wake na maongezi Yake na baraka Zake maalum na kumpatia sehemu kamili ya elimu za ndani za njia Yake. Na Akamjaalia pia zawadi nyingi za mbinguni

na maajabu ya kimbunguni na maarifa na mambo ya ndani ya kiroho ili kwa jiwe hili la kimbunguni sanamu la nta lililotengenezwa kwa “uchawi” wa Kizungu livunjiliwe mbali. Basi enyi Waislamu, kudhihiri kwangu kwa kuondoa magiza ya kiuchawi ni mwujiza kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Je, haikulazimu kwamba kwa kupambana na uchawi, mwujiza pia ungekuja duniani? Je, mnaona jambo hili ni la ajabu na lisilowezekana kwamba Mwenyezi Mungu Aonyeshe mng’ao wa haki wenye athari ya kimwujiza kwa kupambana na udanganyifu wa hali ya juu ulio kama uchawi.

Enyi wenye busara, msione ajabu kwamba Mwenyezi Mungu katika wakati wa haja na katika siku hizi za giza totoro, Ameteremsha nuru ya mbinguni na kumtuma mtu mmoja duniani kwa kumteua kwa masilahi ya watu wote na kwa shabaha ya kuishindisha Islam na kueneza nuru ya yule aliye mbora wa vuimbe vyote na kwa kuwatilia nguvu Waislamu, na pia kwa ajili ya kutakasa hali yao ya ndani. Ajabu ingekuwa kama Mungu Aliye Mlinzi wa dini ya Kiislamu Ambaye Aliahidi kwamba daima Nitakuwa Mwangalizi wa mafundisho ya Kurani na Sitayaacha yadhoofike tena kufisia na kupoteza nuru yake, kwa kuona giza hili na ufisadi wa ndani na nje, Angekaa kimya wala Asingekumbuka ahadi Yake ambayo Alikwisha eleza kwa kusisitiza katika Neno Lake Tukufu. Nasema tena kwamba kama kulikuwa na jambo la ajabu basi lilikuwa ni hili kwamba bishara hii iliyo wazi kabisa ya Mtume Mtukufu s.a.w. ingebatilika ambamo ilinenwa kwamba mwanzoni mwa kila karne, Mwenyezi

Mungu Ataendelea kumwinua mtu ambaye ataijadidisha dini Yake.⁶

⁶ Kueneza tafsiri za Kurani Tukufu kidesturi au kufasiri vitabu vya dini na Hadithi za Mtume s.a.w. kwa Kiurdu au Kiajemi na kuvieneza au kufundisha njia mbovu za bidaa kama ilivyo desturi za masheikh wengi wa zama hizi – hayo si mambo yanayoweza kuhesabiwa kujadidisha dini kikamilifu na kikweli. Bali njia zilizotajwa mwishowe ndiyo kujadidisha njia za Kishetani na ugaidi wa dini. Kueneza Kurani Tukufu na Hadithi zilizo sahihi bila shaka ni njia nzuri, lakini kufanya kazi hii kidesturi na kwa kujikalifisha na kujitahidi pasipo kutenda sawa na Hadithi na Kurani, ndizo huduma za kijuujuu na zisizo na kiini ambazo kila mwenye ujuzi anawenza kuzitoa na sikuzote zinaendelea. Hizo hazina uhusiano wowote na kujadidisha. Mambo haya yote mbele ya Mwenyezi Mungu ni kuuza mifupa tu, si zaidi ya hapo. Mungu Mwenye Enzi Anasema:

لَمْ تَقُولُنَّ مَا لَا تَفْعَلُونَ ① كَبِيرٌ مَّا نَعْدَ اللَّهُ أَنْ تَنْهَوْلُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ②

[Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda. –As-Saf, 61:3-4]

Tena Anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا عَلِمْتُمُ الْفَسَادَ فَلَا يَرْجِعُ كُنْكُنٌ مِّنْ حَلٍ إِذَا افْتَدَيْتُمْ

[Enyi mliaoamini, jiangalieni nafsi zenu. Hatawadhusrungi aliyepeota ikiwa mmeongoka.—Al-Maida, 5:106]

Kipofu atamwonyeshaje kipofu njia na mwenye ukoma atawezaje kutakasa miili ya wengine? Kujadidisha dini ni hali takatifu ambayo kwanza humteremkia kwa jazba ya kimapenzi mwenye moyo safi aliyefikia daraja la kuongea na Mwenyezi Mungu. Halafu hupenya katika wengine upesi au taratibu. Wale wanaojaaliwa nguvu ya kujadidisha toka kwa Mwenyezi Mungu hawawi tu wauza mifupa; bali huwa manaibu wa Mjumbe wa Mungu, na kiroho huwa makhalifa zake. Mwenyezi Mungu Huwarithisha neema zote wanazopewa manabii na mitume. Na mambo yao huwa kwa jazba si kwa kujikalifisha na wanaonyesha matendo, hawasemi maneno matupu. Ufunuo wa Mwenyezi Mungu huziangaza nyoyo zao nao hufundishwa na Roho Mtakatifu katika kila

Basi si jambo la ajabu bali ni la kutoa shukrani mara elfu kwa elfu, na ni wakati wa kuongeza imani na yakini kwamba Mwenyezi Mungu kwa fadhili na ukarimu Wake, Ametimiza ahadi Yake na Hakuahirisha hata kwa dakika moja kutimiza bishara ya Mtume Wake. Na si tu kwamba Ametimiza bishara hiyo, bali Amefungua mlango wa maelfu ya bishara na miujiza kwa siku zijazo. Kama m waamnio, basi shukuruni na fanyeni sujuda za shukrani kwamba zama ambazo mababu zenu walifariki wakizisubiri, na roho nydingi ziliaga dunia zikiwa na shauku ya kuzipata, nyinyi mmezipata. Sasa kuzithamini au kutozithamini na kufaidika nazo au kutofaidika nazo ni hiari yenu. Mimi siwezi kujizuia kueleza kwamba mimi ndimi niliyetumwa katika wakati hasa kwa kuwarekebisha wanadamu ili kuimarisha upya dini miyoni. Mimi nimetumwa kama alivyotumwa yule mtu, baada ya mja wa Mungu Kalimullah [Musa a.s.], ambaye roho yake katika enzi ya Herode ilinyayuliwa mbinguni baada ya mateso mengi. Basi Kalimullah wa pili (Mtume s.a.w.) ambaye kwa hakika ni wa kwanza kabisa na ni Mkuu wa manabii wote, alipokuja kuwaponda vichwa Mafirauni wengine ambaye kumhusu yeche imesemwa

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ

كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْ فِرْعَوْنَ رَسُولًا ٧

mushkili. Na katika maneno na mienendo yao hamna mchanganyiko wa mapenzi ya dunia, kwani wametakaswa kabisa na kuvutwa kwenye Mungu kitimilifu na kikamilifu (Mwandishi).

⁷ Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni. –Al-Muzzammil, 73:16

ye ye naye aliyefanana na Kalim wa kwanza katika kazi zake lakini alikuwa mtukufu zaidi kuliko yeye katika daraja, akaahidiwa ujaji wa mfano wa Masihi. Na huyo mfano wa Masihi akipata nguvu na tabia na sifa za Masihi mwana wa Mariamu, ameteremka toka mbinguni katika zama kama zile na katika muda karibu ule ule uliokuwa baina ya zama za Kalim wa kwanza na Masihi mwana wa Mariamu, yaani karne ya kumi na nne. Na kuteremka kuko kulikuwa ni kwa kiroho kama watu waliokamilika baada ya kupaa hutaremka kwa kuwarekebisha viumbe wa Mungu. Na ameteremka katika zama zinazofanana, katika mambo yote, na zama za kuteremka kwa Masihi mwana wa Mariamu, ili iwe ishara kwa wenye kufahamu.⁸

⁸ Zama hizi tulizomo humu ni zama ambamo kuchukua mambo kidhahiri na kuwa mbali na kiini na uhakika, na ukosefu wa uaminifu na amana, na kuachana na ukweli na khulka njema, na wingi wa tamaa na ubahili na huba ya dunia, vimeenea sana kama vilivyoenea katika Mayahudi wakati alipodhahiri Masihi mwana wa Mariamu. Basi kama ambavyo Mayahudi katika zama hizo walikuwa hawana habari kabisa ya wema wa kweli na wakafahamu mila na mazoea tu kuwa ndio wema, na zaidi ya hayo uaminifu na amana na utakaso wa ndani na uadilifu vikatoweka kabisa kati yao wala haikubaki hata alama ya huruma na rehema ya kweli, na ibada ya aina mabalimbali ya viumbe ikashika nafasi ya Mwabudiwa wa kweli, ndivyo yalivyodhahirika mabalaa hayo yote katika zama hizi. Vitu vilivyo halali havitumiwi kwa shukrani na unyenyekevu wenye shukrani. Haikubaki karaha wala chuki kuyatenda yaliyoharimishwa. Amri kubwa za Mwenyezi Mungu zinawekwa kando kwa maelezo mabovu. Wanazuoni wengi wa zama zetu pia hawatofautiani na Waandishi na Mafarisayo wa zama hizo. Wanachuja mbu na kumeza ngamia. Wanawafungia watu ufalme wa mbinguni. Wenyewe hawaingii humo wala hawawaruhusu wanaotaka kuingia

humo. Wanasali sala ndefu ndefu lakini moyoni hamna mapenzi wala taadhima ya Yule Mwabudiwa wa kweli. Wakiketi juu ya mimbari hutoa mawaidha yenye msisimko lakini shughuli zao za ndani ni tofauti kabisa. Ni ya ajabu macho yao kwamba juu ya kuwa na uasi wa miyo yao na ufisadi wa nia yana ufundi mkubwa wa kulia. Ni za ajabu ndimi zao kwamba juu ya miyo yao kuwa na ugeni sana, zinadhihirisha urafiki. Halikadhalika, tabia za Kiyahudi zinaonekana zikienea kila upande. Wema na ucha-Mungu umepungua sana. Udhaiju wa imani umeyapoza mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Watu wanazama ndani ya mapenzi ya dunia, na ilikuwa ni lazima iwe hivyo, kwani Mtukufu Seyyidna wa Maulana s.a.w. amekwisha tabiri kwamba zitaufikia umati huu zama ambamo watajifananisha kabisa na Mayahudi, nao watatenda yote waliyoyatenda Mayahudi kiasi hiki kwamba hata kama Mayahudi waliingga ndani ya tundu la panya basi nao pia wataingia. Ndipo mionganoni mwa Waajemi atatokea mtu atakayefundisha imani, na hata kama imani itungikwe kwenye kilimia basi ataipata kutoka huko. Hii ni bishara ya Mtume s.a.w. ambayo ufunuo wa Mwenyezi Mungu umenifunulia uhakika wake na kudhihirisha wazi kaifa yake. Na Mwenyezi Mungu Alinifunulia kwa wahyi Wake kwamba hata Masihi mwana wa Mariamu kwa hakika alikuwa ni mwenye kufundisha imani ambaye alizaliwa miaka elfu moja mia nne baada ya Nabii Musa a.s. katika zama ambapo hali ya kiimani ya Mayahudi ilidhoofika sana, nao kwa sababu ya udhaifu wa imani wakanasa katika maovu yote ambayo kwa hakika ni matawi ya ukosefu wa imani. Hivyo, baada ya kupita muda wa miaka karibu elfu moja mia nne tangu kutumwa kwa Nabii wake s.a.w. maafa hayo yalitokea sana kati yao ambayo yalitokea katika Mayahudi ili bishara iliyotolewa kuwahuusu itimie. Basi Mwenyezi Mungu Aliwatumia mfano wa Masihi mwenye kufundisha imani kwa kudra Yake. Masihi aliyetabiriwa kuja ndiye huyu; mkitaka mkubalini. Mwenye masikio na asikie. Hii ni kazi ya Mwenyezi Mungu na ni ajabu machoni mwa watu. Na kama yejote alikadhibishe jambo hili, basi hata wakweli wa zamani nao walikadhibishwa. Yohana yaani Yahya aliyejewa mwana wa Zakaria hakupokelewa na Mayahudi hata kidogo, ilhali Masihi alitoa ushuhuda kumhusu yeje

kwamba ndiye aliyenyanjiliwa mbinguni ambaye kushuka kwake tena kutoka mbinguni kuliahidiwa katika maandiko matakatifu. Mwenyezi Mungu daima Hutumia istiara na kulingana na tabia na sifa na kipawa Humpatia mtu jina la mwagine. Yule aliye na moyo unaolingana na moyo wa Ibrahimu ndiye Ibrahimu mbele ya Mwenyezi Mungu na mwenye moyo wa Umar Faruk ndiye Umar Faruk mbele ya Mwenyezi Mungu. Je, hamsomi Hadithi hii kwamba kama katika umati huu wako Muahaddathina ambao Mwenyezi Mungu Anaongea nao basi ndiye Umar r.a. Je, Hadithi hii inamaanisha kwamba sasa Umuhaddathi umeishia kwa Hadhrat Umar r.a. hata kidogo. Bali muradi wa Hadithi ni kwamba mtu ambaye hali yake ya kiroho imelingana na hali ya kiroho ya Umar r.a. ndiye atakayekuwa Muahaddath wakati wa haja. Mimi nami nilifunuliwa

فِيَكَ مَادَّةٌ فَأَرْوَقِيَّةٌ

[Una tabia ya Kifaruki]. Hivyo, mimi zaidi ya kufanana na watakatifu wengine kitabia, ambako maelezo yake yote yameandikwa kikamilifu katika *Barahine Ahmadiyya*, nina mshabaha maalum na tabia ya asili ya Masihi a.s. Na kwa sababu ya mshabaha huo wa kitabia, nimetumwa kwa jina la Masihi ili itikadi ya msalaba ivunjiliwe mbali. Hivyo, nimetumwa kwa kuvunja msalaba na kuua nguruwe. Nimeshuka kutoka mbinguni pamoja na Malaika watakatifu waliokuwa kulia na kushoto kwangu ambao Mungu wangu Aliye pamoja nami Atawaingiza katika kila moyo mwelekevu, bali Anaendelea kufanya hivyo. Na hata kama nikae kimya na kalamu yangu iache kuandika, hata hivyo Malaika walioteremka pamoja nami hawawezi kuacha kufanya kazi yao, na mikononi mwao mna marungu makubwa makubwa waliyopewa kwa kuvunja msalaba na kuponda hekalu la ibada ya viumbe. Pengine asiyejua atashangaa kwamba kuteremka Malaika kuna maana gani. Basi ibainike kwamba suna ya Mwenyezi Mungu ndiyo hii kwamba pindi anaposhuka toka mbinguni Mtume au Nabii au Muahaddath kwa kuwarekebisha viumbe wa Mwenyezi Mungu, basi hushuka pamoja naye Malaika wanaotilia mwongozo katika miyo iliyo tayari kuupokea na kuhimiza kutenda wema, na huwa wanafululiza kuteremka hadi giza la ukafiri na upotevu litoweke na alfajiri ya imani na ukweli ipambazuke kama Asemavyo Mwenyezi Mungu Mwenye shani:

تَنْزِيلُ الْمَلِكَةِ وَالرُّوحُ فِيهَا يَذِينُ رَبِّهِمْ مَنْ كُلِّ أَمْرٍ ثُمَّ سَلَمَ هِيَ حَلِيَّةٌ مُطْلَعٌ اَنْفَجِيرٌ

[Huteremka Malaika na ufunuo katika huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. Amani; na (usiku) huo (unaendelea) mpaka mapambazuko ya alfajiri.—Al-Kadr, 97:5-6]

Basi ushukaji wa Malaika na Roho Mtakatifu, yaani kuteremka kutoka mbinguni huwa wakati mtu mwenye shani kubwa akivaa joho la Ukhalifa na kufunuliwa na Mwenyezi Mungu anaposhuka ardhini. Ama Roho Mtakatifu, Khalifa tu ndiye anapatiwa, na Malaika walio pamoja naye huteremshwa katika miyo myelekevu duniani kote. Hapo, popote pale duniani wapatikanapo waelekevu, huathirika na mwanga huo, na ulimwenguni kote mng'ao wake huenea, na kwa athari takatifu ya Malaika, mawazo mema huanza kuzalika yenyewe ndani ya miyo na Umoja wa Mungu huanza kupendeza na nyoyo nyofu hupulizwa roho ya kupenda ukweli na kutafuta haki, na wanyonge hupewa nguvu, na kila upande upopo huanza kuvuma ambao humsaidia Msuluhihi katika shabaha na makusudio yake. Kwa mkono uliofichikana, watu wenyewe wanaskumwa kwenye wema, na mataifa yanaanza kupata msisimko. Hapo watu wasiofahamu wanadhani kwamba nadharia za dunia zimegeuka zenyewe tu kwenye ukweli, lakini kwa hakika kazi hiyo huwa ya Malaika ambao huteremka kutoka mbinguni pamoja na Khalifa wa Mungu na huwatolea watu uwezo usio wa kawaida wa kuikubali haki na kuifahamu, huwaamsha waliolala, huwazindua waliolewa, huwafungulia masikio viziwi, huwapulizia wafu roho ya uhai na huwatoa nje waliomo makaburini. Ndipo mara watu wanaanza kufumbua macho na mambo yaliyofichika hapo kabla huanza kufichuka kwa miyo yao. Na kwa hakika Malaika hao hawatengani na Khalifa huyo wa Mwenyezi Mungu. Wao huwa nuru ya uso wake na athari dhahiri za bidii yake, ambao kwa nguvu yao ya kisumaku humvutia kila anayehusiana nao, awe karibu kimwili au mbali, na awe anamjua au hamjui kabisa hata asijue jina lake. Ilmuradi, katika zama hizo maelekeo yoyote kwenye wema na jazba zinazalika kwa kupokea ukweli; hata kama hizo zizalike katika Waasia au Wazungu au

Waamerika, hizo kwa hakika hudhihirika kwa kuhimizwa na Malaika wanaoteremka pamoja na Khalifa huyo wa Mwenyezi Mungu. Hii ni kanuni ya Mwenyezi Mungu ambamo kamwe hamtapata mabadiliko nayo ni wazi kabisa na upesi kufahamika na ni bahati yenu mbaya msipoitafakari. Kwa kuwa nimetoka kwa Mwenyezi Mungu na unyofu na ukweli, hivyo mtazipata ishara za ukweli kutoka kila upande. Wakati hauko mbali, bali u karibu sana ambapo mtaona majeshi ya Malaika yakishuka kutoka mbinguni na kuiteremka mioyo ya Asia na Ulaya na Amerika. Mmekwisha jua kutoka katika Kurani Tukufu kwamba Khalifa wa Mungu akishuka ni lazima Malaika washuke pamoja naye ili waielekeze mioyo kwenye haki; hivyo ingojeni ishara hii. Wasiposhuka Malaika na msipoona athari wazi za kuteremka kwao na msipokuta mioyo kuelekea kwenye haki zaidi ya kawaida, basi fahamuni kwamba hakuna ye yote alireshuka kutoka mbinguni. Lakini kama mambo hayo yote yakinoteka, hapo msikatae ili msihesabiwe waasi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Ishara ya pili ni hii kwamba Mwenyezi Mungu Ameniteua kwa nuru wanazojaaliwa wateule ambazo katika hizo wengine hawawezi kushindana. Basi kama mna shaka, njoni kushindana nami na fahamuni kwa yakini kwamba hamtaweza kamwe kushindana. Mnazo ndimi lakini mioyo hamna; mwili upo lakini roho hakuna; mboni za macho zipo lakini nuru hamna. Mwenyezi Mungu Awajaalieni nuru mkaone.

Ishara ya tatu ni hii kwamba yule Nabii Mteule ambaye mnadai kumwamini, Nabii huyo Mtukufu a.s. ametoa habari kunihusu mimi ambayo imo katika vitabu vilivyo Sahihi vya Hadithi, lakini hamjaizingatia mpaka leo. Basi ninyi kwa hakika m maadui wa siri wa Mtume s.a.w. kwamba mnajaribu kumkadhibisha si kumsadikisha. Sasa wengi wenu wataandika fatuwa ya kunikufurisha na kama ingewezekana wangeniu. Lakini serikali hii si serikali ya watu wenye kuchocheka haraka na wabovu wa kufahamu na walio nyuma sana katika khulka ya kuvumilia na wenye kuhuisha roho ya Kiyahudi. Ingawa serikali hii haina fadhila na baraka za imani, hata hivyo ni bora sana kuliko

enzi ya Herode ambayo Masihi bin Mariamu a.s. alikabiliana nayo na ni afadhali sana kuliko serikali za Kiislamu za siku hizi katika kuleta amani na kustawisha jamii na kutoa uhuru na kulinda na kuwaelimisha raia na kusimamisha sheria ya uadilifu na kuwaadhibu wahalifu. Jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu kwa hekima Yake nyingi hakumtuma Masihi katika siku za utawala wa Mayahudi na chini ya serikali yao, ndivyo ilivyotumiwa hekima hiyo kunihusu mimi ili iwe ishara kwa wenyewe kufahamu. Kama wakataaji wa zama hizi wakinidhishaki basi si jambo la kusikitisha kwani waliowatangulia waliwatendea Manabii wa zama zao vibaya zaidi kuliko hao. Masihi a.s. naye alichewka mara nyingi na kufanyiwa dhihaka. Safari moja ndugu zake waliozaliwa katika tumbo moja walitaka kwamba wakimchukulia mwendawazimu wamfungishe jela. Ama watu wengine, mara nyingi walidhamiria kumwua na wakamtupia mawe na wakidharau wakamtemeaa mate ya uso. Bali safari moja walimtundika msalabani na wakadhani wamemwua. Lakini kwa kuwa mifupa haikuvunjwa, hivyo akasalimika kwa msaada wa mtu mwema mwenye kumwamini, na baada ya kuishi siku zilizosalia za maisha yake akanyanyuliwa mbinguni. Wafuasi na marafiki wa karibu wa Masihi a.s. nao wakateleza. Mmoja alichukua rushwa ya rupia thelathini na kumkamatisha na mwingine akimwashiria akamlaani, na wanafunzi wengine ambao walijidai kuwa marafiki wakamkimbia na wakaingiwa na shaka za aina mbalimbali kumhusu Masihi a.s. Lakini kwa kuwa yeye alikuwa mkweli, hivyo Mwenyezi Mungu Akahuisha tena kazi yake iliyokuwa imekufa. Uhai wa mara ya pili wa Masihi a.s. unaoaminiwa na Wakristo kwa hakika unaashiria kwenye uhai wa dini yake ambayo ilihuisha tena baada ya kuwa imekufa. Halikadhalika, Mwenyezi Mungu Amenipa mimi pia habari njema kwamba ‘Nitakujaalia uhai baada ya kufa.’ Na Akasema kwamba waliomkurubia Mwenyezi Mungu huhuika baada ya kufa. Na Akasema: Yaani, Mimi Nitaonyesha mnga’o Wangu na Nitakunyanya kwa kuonyesha kudra Yangu.

Hivyo, muradi wa uhai wangu huu wa mara ya pili ni uhai wa makusudio yangu lakini ni wachache wanaozifahamu siri hizo. Basi. – Mwandishi

Hivyo kila mmoja anapaswa asifanye haraka kumkataa asiye akawa anapigana na Mwenyezi Mungu. Watu wa dunia ambao wameimarika katika mawazo mapotovu na fikira za zamani hawatamkubali lakini karibuni zitakuja zama zitakazowadhihirishia kosa lao.

Mwonyaji mmoja alikuja duniani, lakini dunia haikumpokea, bali Mungu Atampokea na kwa mashambulio makali Atadhihirisha ukweli wake. Hii si kauli ya mwanadamu, ni ufunuo wa Mwenyezi Mungu na maneno ya Mola Mwenye Jalali. Nami nina yakini kwamba siku za mashambulizi hayo ni karibu. Lakini mashambulizi hayo hayatakuwa ya upanga na shoka na hakutakuwa na haja ya mapanga na mabunduki, bali kwa silaha za kiroho msaada wa Mwenyezi Mungu utateremka na kutakuwa na mapigano makali na Mayahudi. Hao ni akina nani? Ni watu wa zama hizi wanaochukua muradi wa kidhahiri ambao wamezifuata nyayo za Mayahudi hatua kwa hatua. Upanga wa kimbunguni wa Mungu utawakata hao wote vipande viwili na tabia ya Kiyahudi itafutwa. Na kila mficha haki, Dajjal, mwenye kuiabudu dunia, mwenye chongo asiye na jicho la kidini atauliwa kwa upanga wa hoja madhubuti na ushindi wa ukweli utapatikana, na siku ile ya ustawi na mnga'o wa Islam itakuja tena kama ilivyokuja zamani, na juu lile litachomoza tena kwa ukamilifu wake wote kama lilivyochomoza hapo awali. Lakini bado. Ni lazima mbingu ilizuie kuchomoza mpaka kwa bidii na jitihada tutokwe jasho na tutengane na raha zote ili litokee, na tukubali dhila zote kwa heshima ya Islam. Kuhuika Islam

kunataka tutoe fidia. Ni nini hiyo? Tufe katika njia hii hii. Ndicho kifo ambacho unakitegemea uhai wa Islam, uhai wa Waislamu na maonyesho ya Mungu Aliye Hai; ndicho kitu ambacho kwa maneno mengine huitwa Islam. Hiyo Islam Mwenyezi Mungu Anataka kuihuisha sasa. Na ilikuwa ni lazima kwamba kwa kutekeleza kazi hii kubwa Yeye Angeanzisha mpango mkubwa sana ambao uwe na athari kwa kila jiha. Basi Mungu Mwenye hekima na Mweza Akinituma kwa kuwarekebisha wanadamu, na kuivuta dunia kwenye haki na ukweli, Akaigawa katika matawi kadha kazi ya kuisaidia haki na kuieneza Islam. Basi miongoni mwa matawi hayo, **tawi mojawapo** ni kazi ya kutunga na kuandika vitabu, ambayo nimekabidhiwa mimi. Na nimefundishwa maarifa na elimu za ndani ambazo haziwezi kujulikana kwa uwezo wa mtu, bali kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tu pekee, na si kwa mtu kujikalifisha, bali kwa kufundishwa na Roho Mtakatifu matatizo yakatatuliwa.

Tawi la pili la Mpango huu ni shughuli ya kutoa matangazo ambayo kwa amri ya Mungu inaendelea kwa shabaha ya kutimiza hoja, na hadi sasa zaidi ya matangazo elfu ishirini yamekwisha enezwa ili kukamilisha hoja za Kiislamu kwa wafuasi wa dini nyingine na daima yataendelea katika nyakati za haja.

Tawi la tatu la Mpango huu ni wageni na wasafiri watafutao ukweli na wajao kwa shabaha mbalimbali ambao wakipata habari ya Mpango huu wa kimbunguni wanawasili kwa

nia ya kuonana nami. Tawi hili pia linaendelea kustawi, ingawa siku fulani hupungua lakini siku nyingine huja kwa wingi sana. Pengine katika miaka hii saba wageni zaidi ya elfu sitini walikuja, na kiasi walichonufaishwa waelekevu mionganoni mwao kwa njia za hotuba na kutatuliwa matatizo yao na kuondolewa udhaifu wao, Mungu Anajua. Lakini hakuna shaka kwamba hotuba hizi zilizotolewa au zinatolewa kujibu maswali ya waulizaji au yanayoelezwa sawa na hali, ni njia ambayo imethhibitika wakati mwingine ya kufaa na kuathiri na kueleweka haraka kuliko vitabu. Ndiyo sababu Manabii wote walitumia njia hii. Na kwa kuacha maneno ya Mwenyezi Mungu ambayo hususan yaliandikwa na kuenezwa, maneno yote ya Manabii yaliendelea kuenea sawa na hali kama hotuba. Desturi ya Manabii kwa jumla ilikuwa ni hii kwamba kama mhadhiri ajuaye kutumia vema fursa, walikuwa wakitoa hotuba kwa kupata nguvu kutoka Roho katika nyakati za mahitaji kwenye vikao na mahafali mbalimbali kulinga na hali yao. Lakini si kama wataalamu wa falsafa wa siku hizi ambao kwa hotuba zao wanakusudia kuonyesha ujuzi wao tu; au huwa na shabaha ya kumrubuni juha fulani kwa mantiki yao ya uwongo na hoja za ovyo na kumfanya kuwa mwenye kustahiki zaidi kuliko wao wenyewe kwenda Jahanamu. Bali Manabii walikuwa wanaongea bila kujikalifisha, na chochote kilichobubujika miyoni mwao wakatilia nyoyoni mwa wengine. Maongezi yao matakatifu yalikuwa katika mahali pafaapo na wakati wa haja; hawakuongea na wasikilizaji kwa kuwaburudisha au kusimulia hadithi za kubuniwa, bali kwa kuwaona ni wagonjwa na kuwakuta wakikumbwa na maafa ya aina

mbalimbali ya kiroho wakawasihi au wakawaondolea wasiwas i wao kwa hoja madhubuti. Na maongezi yao yalikuwa na maneno machache lakini maana nyingi. Basi mimi nami naifuata desturi hiyo na sawa na vipawa na mahitaji ya wageni na kwa kuangalia maradhi yao maongezi yanaendelea daima.⁹ Kwani baada ya kuona uovu, kutoa nasaha zinazohitajika ili kuuzuia, na kuzirekebisha khulka zilizoharibika, ndiyo tiba inayowezekana katika hali iwapo mgonjwa yupo mbele wala haiwezekani ipasavyo katika hali yoyote nyingine. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Aliwatura maelfu ya Manabii na Mitume na Akaagiza kukaa pamoja nao ili watu wa kila zama wajionee wenyewe mifano, na kwa kuwashuhudia kwamba hao ndio Wahyi wa Mungu kwa sura ya kiwiliwili wajaribu kuwafuata. Kama kukaa pamoja na watu wema hakungekuwa katika wajibu wa dini, Mwenyezi Mungu Angeweza kuteremsha maneno Yake

⁹ Hapa kuna kisa cha ajabu kinachostahili kuandikwa kwamba safari moja niliwahi kwenda Aligarh na kutokana na udhaifu wa ubongo ambaa ulinisibu hapo kabla nilipokuwa Qadian nikawa siwezi kuongea sana wala kufanya kazi ya kuchosha sana ubongo, na hata sasa hali yangu ndiyo hii kwamba siwezi kuongea sana na kutafakari. Katika hali hii Sheikh mmoja wa Aligarh, jina lake Muhammad Ismail, akaonana nami na kuniomba kwa unyenyekevu sana kutoa waadhi. Akasema kwamba tangu muda mrefu watu wana shauku ya kukusikiliza, hivyo ni vizuri watu wote wajumuike mahali fulani na utoe waadhi kidogo. Kwa kuwa sikuzote nilikuwa na upendo na hamu ya kuwaeleza watu maneno ya haki, hivyo nikakubali ombi hilo kwa shauku ya moyo na nikataka kuwaeleza watu hadharani uhakika wa Islam kwamba Islam ni kitu gani na watu sasa wanaifahamuje. Na bwana Sheikh akaambiwa

pia kwamba Mungu Akijaalia uhakika wa Islam utaelezwa. Lakini baadaye nikazuwa na Mwenyezi Mungu. Nina yakini kwamba kwa kuwa hali yangu ya afya haikuwa nzuri, ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Hakutaka nipaye maradhi kwa kufanya kazi ya kuchosha sana ubongo, hivyo Akanizua kutoa waadhi. Hapo kabla pia safari moja ilitokea hivi kwamba katika hali yangu ya udhaifu, Nabii mmojawapo mionganoni mwa Manabii wa zamani akaonana nami katika hali ya kashfi na akinihurumia na kunisihi akasema: Kwa nini unafanya kazi ya kuchosha sana ubongo, hiyo itakufanya uuque. Kwa vyovyote hicho kilikuwa ni kizuizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Sheikh huyo akapashwa habari ya udhuru huo na kwa hakika udhuru huo ulikuwa wa kweli. Wale walioona mashambulizi makali ya ugonjwa wangu huu baada ya kuongea sana na kutafakari mno, ingawa kwa sababu ya kutokunjuwa hawaziamini funuo zangu, lakini watakuwa na yakini kamili kwamba kwa hakika mimi ninayo maradhi hayo. Dkt. Muhammad Husain, ambaye pia ni hakimu kiheshima huko Lahore na hadi sasa ananitibu, sikuzote anasisitiza kwamba nijiepushe na kazi za kuchosha sana ubongo maadamu yapo maradhi haya. Na bwana daktari huyo ni shahidi wa kwanza wa hali yangu hii, na marafiki zangu wengi kama vile ndugu yangu Maulawii Hakim Nuruddin aliye tabibu wa serikali ya Jammu, ambaye daima hushughulika kunihudumia kwa moyo wote, na Munshi Abdul Haq mhasibu aishiye mjini Lahore na kufanya kazi huko ambaye alinihudumia katika ugonjwa wangu huu hata kwamba siwezi kuieleza huduma hiyo, hao waaminifu wangu wote ni mashahidi wa hali yangu hii. Lakini ni masikitiko kwamba ingawa kila mwaminio anatakiwa awe na dhana njema, lakini Sheikh huyo hakukubali udhuru huo akiwa na dhana njema, bali akifanya dhana mbaya kupita kiasi akauona ni uwongo. Basi hotuba yake yote ambayo daktari moja rafiki yake, jina lake Dkt. Jamaluddin, akaianika kwa idhini yake na kuieneza katika watu, naiandika hapa chini pamoja na jibu lake:

Kauli Yake (Sheikh Muhammad Ismail): Mimi nilimwambia (yaani mimi huko Aligarh) kwamba kesho ni Ijumaa, utoe waadhi. Akaahidi lakini asubuhi ikaja barua kwamba kwa ufunuo nimekatazwa kutoa

waadhi. Nadhani alikataa kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kujieleza na kwa kuogopa mtihani.

Jibu Langu: Dhana hii ya Sheikh huyo haina ukweli wala uhakika wowote isipokuwa ni dhana mbaya tu ambayo ni mionganini mwa mambo yaliyokatazwa vikali na sheria wala si kazi ya watu wenyewe tabia njema. Kama ningedai ya kwamba nimeanza kupata ufunuo mara baada ya kuja Aligarh, hapo bila shaka kungeweza kuwa na sababu ya kufanya dhana mbaya, na bila shaka ingeweza kufikiriwa kuwa mimi kwa kuona daraja la juu la utaalamu wa Sheikh na adhama na heba ya sifa zake, nikiathirika nikafadhaika, na kwa kutoa udhuru na kuzusha hila nikakimbia. Lakini mimi nimekwisha tangaza kote nchini madai yangu ya kufunuliwa miaka sita kabla ya safari ya Aligarh, na sehemu nyingi za *Barahin-e-Ahmadiyya* zimejaa funuo. Kama nisingekuwa na uwezo wa kutoa hotuba basi vitabu vilivyoandikwa na kuenezwa ambavyo ni hotuba zangu nilizotoa katika hafla na mkutano wa maelfu ya marafiki na wapinzani, kama vile *Surma Chashme Arya*, vingewezekanaje kwa uwezo wangu dhaifu wa kuongea? Na ningewezaje kuendelea na mfululizo wa hotuba kabambe hadi leo ambamo hulazimika kuchosha ubongo kwa kufahamisha maelfu ya watu wenyewe tabia na vipawa tofauti. Nawasikitikia mara elfu masheikh wengi wa zama hizi kwamba wameliwa ndani kwa ndani na moto wa husuda. Kwa watu wanatoa mawaiida kuwa na sifa za imani na kutendeana kidugu na kudhaniana vyema na wakipanda majukwaani huwasomea aya za Neno la Mungu kuhusu habari hii, lakini wenywewe hawazisogelei karibu amri hizi. Ee bwana! Mwenyezi Mungu Akufumbulie macho. Je, haiwezekani kwamba Mwenyezi Mungu kwa masilahi fulani Amzuie mja Wake afunuliwaye kufanya kazi fulani? Na huenda sababu ya pili ya kuzuia ni kwamba tabia zako za ndani zitahiniwe, na waliofanana nawe katika khulka na tabia uchafu wao utoke nje kwa njia hii. Ama mimi kuogopa adhama na heba ya elimu yako, basi ujue kwa yakini kwamba wale waliomo gizani na kunaswa katika magiza ya kinafsisi wamejikusanya falsafa na sayansi zote za dunia, hata hivyo kwangu mimi hawana thamani zaidi ya mdudu aliyekufa. Lakini huna hata kiwango hicho

cha elimu. U Sheikh mkavu mwenye mawazo ya zamani na ndani mwako mna udhalili ule upatikanao katika masheikh wenyewe mawazo mabovu. Na uzingatie kwamba mara nyingi wanijia wahakiki na wenyewe fani na wajuzi wa mambo mengi na kufaidika na maarifa ya ndani hata kwamba kama nikuita mtoto wa shulenii, kwa maneno hayo nitakuwa nimekupa heshima usiyostahiki. Na kama bado wasiwasi wako hautoweki na maono ya dhana mbaya hayafifii basi kwa msaada na rehema ya Mwenyezi Mungu nipo tayari kushindana nawe katika kutoa hotuba. Mimi kwa sababu ya maradhi siwezi sasa kwenda safari ya mbali. Lakini kama waridhia basi nipo tayari kukutolea nauli ya kufika mji kama Lahore, makao makuu ya Panjab, kwa kazi hii na mtihani huu, na ninatoa ahadi hii kwa uthabiti, nami nasubiri jibu lako.

Kauli Yake: Huyu mtu ni mzito wa akili, hana elimu.

Kauli Yangu: Ee bwana! Mimi sidai kuwa na hekima na busara yoyote ya dunia. Nifanye nini na busara na hila za dunia hii kwani haziwezi kunawirisha roho, haziwezi kusafisha uchafu wa ndani wala haziwezi kuleta unyenyekevu bali zinatia kutu juu ya kutu na kuongeza kufuru juu ya kufuru. Kwangu yatosha tu kwamba Mwenyezi Mungu Amenisa idia kwa fadhili Yake na Amenijaalia elimu ambayo hupatikana si vyuoni bali kutoka kwa Mwalimu wa mbinguni. Kama nikiitwa Ummi (asiyejua kusoma na kuandika) sivunjiki heshima bali ni fahari kwangu, kwani Kiongozi wangu na wa viumbe wote wa Mwenyezi Mungu ambaye alitumwa kuwarekebisha wanadamu wote naye alikuwa Ummi. Mimi kamwe sitalihesabu fuvu la kichwa lile linalojivunia elimu lakini njie yake na undani wake umejaa giza. Fungua Kurani ukatafakari mfano wa punda, je hautoshi?

Kauli Yake: Nilimwuliza masawali machache kuhusu ufunuo. Akitoa majibu kidogo yasiyo na maana akanyamaza.

Jibu Langu: Nakumbuka, majibu ya maana sana yalitolewa yaliyomtosha mtu mwenye akili kidogo na mwadilifu lakini wewe hukuelewa. Sasa ni nani aliyevunjika heshima, wewe au mwingine? Hebu toa maswali hayo katika gazeti lolote ukajaribiwe tena kujidhania kwako vema.

Kauli Yake: Haiwezi kuyakinika hata kidogo kwamba vitabu vizuri kama hivyo vimetungwa na bwana huyu.

Jibu Langu: Utayakinije? Yakini hiyo hawakuipata hata makafiri waliomwona Mtume s.a.w. kwa macho yao wenyewe na kwa sababu ya miyo yao kufunikwa sana, sifa bora za Mtume s.a.w. hazikuweza kuwafunukia na wakaendelea kusema kwamba maneno haya fasihi yanayotoka kinywani mwake na Kurani hii anayowasikilizisha watu, ibara zote hizi kwa hakika ni utunzi wa watu wengine anaofundishwa asubuhi na jioni. Na kwa maana fulani makafiri hao pia walisema kweli na Sheikh naye amesema sawa, kwani bila shaka maneno ya Kurani Tukufu, kwa ufasaha na hekima, yako juu sana ya uwezo wa kiakili wa Mtume s.a.w., bali yako juu na bora zaidi kuliko uwezo wa viumbe wote, na maneno hayo hayawezi kuwa ya mwingine minghairi ya Mjuzi wa kila kitu na Mwenye uwezo kamili. Halikadhalika, vitabu nilivyotunga na kuvichapa, hivyo vyote kwa hakika ni matokeo ya msaada wa Mugnu na ni zaidi ya uwezo wa ujuzi wangu.

Namshukuru Mungu kwamba kwa kukosoa kwa Sheikh huyo imetimia bishara moja iliyomo katika *Barahin-e-Ahmadiyya* kwamba baadhi ya watu kwa kusoma kitabu hiki watasema kwamba hiki hakikutungwa na mtu huyu

Bali walimsaidia juu yake watu wengine. [Tazameni *Barahin-e-Ahmadiyya* uk. 239]

Kauli Yake: Seyyid Ahmad, Mwarabu, ambaye nionavyo ni mtu wa kutegemewa, aliniambia mwenyewe kwamba: Mimi nilikaa kwake kwa

miezi miwili katika kundi la wafuasi wake maalum na nikahudhuria mara kwa mara katika wakati maalum kwa shabaha ya kupeleleza na kutafiti na nikachunguza na kujua kwamba kwa hakika ye ye anavyo vyombo nya unajimu, naye huvitumia.

Jibu Langu:

عَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَمَوْلَانَا وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَمَوْلَانَا وَأَنْفَسَنَا
وَأَنْفَسَكُنْدُرٌ مَمَّا تَبَرَّأْ فَنَجَّعْلُ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكُذَّابِينَ ⑤

[Njoni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na watu wetu na watu wenu; kisha tuombe kwa unyenyekevu na kuiweka laana ya Mwenyezi Mungu juu ya waongo. –Aali ‘Imran, 3:62]

Jibu Langu kwa hakika ndilo niloliandika kwa kutoa aya ya Mwenyezi Mungu, nami sikumbuki hata kidogo kwamba huyo seyyid Ahmad ni mzee gani aliyekaa kwangu kwa miezi miwili. Ni jukumu la Sheikh kumleta kwangu ili aulizwe ni vyombo vipi alivyovishuhudia. Maadamu nipo hai hadi sasa, Sheikh mwenyewe akae pamoja nami miezi miwili na kujiona mwenyewe, kuna haja gani ya kumtia Mwarabu au Mwajemi katikati.

Kauli Yake: Kwa kuyatafakari maneno ya ufunuo, siyakini hata kidogo kama hayo kweli ni ufunuo.

Jibu Langu: Hata wale pia hawakupata yakini ambao kuwahuusu hao Mwenyezi Mungu Anasema:

وَكَذَّبُوا بِإِيمَانِنَا كَذَّابًا ط

[Walikadhibisha sana Aya Zetu. –An-Naba’, 78:29]

Firauni hakupata yakini; waandishi na mafarisayo wa Mayahudi hawakupata yakini; Abu Jahli na Abu Lahab hawakupata yakini. Bali wale walipata yakini waliokuwa wanyonge na waliotakasika.

Bahati hii njema haiwi kwa nguvu ya mtu, Asipojaalia Mungu Mpaji.

Kauli Yake: Kudai kufunuliwa ni kinyume na karama na ni madai batili kusema kwamba anayekataa aje mwenyewe kujionea.

Jibu Langu: Mambo haya si ya binadamu bali ni kutoka kwa Yule Ambaye madai yote yanamfikia. Basi ni mtu gani wa haki anayeweza kusema ni batili. Naam, ni kweli kwamba kudai jambo lililo kinyume na kawaida hata Nabii ye yote haliwezi. Lakini, je, haijuzu kwa Mwenyezi Mungu pia kudai madai kama haya kwa njia ya Nabii au Mtume au Muhaddath?

Kauli Yake: Baada ya kuonana naye sina imani naye tena. Nionavyo mimi, ye yote anayemwamini Mungu Mmoja akionana naye hatakuwa na imani naye tena. Anaahirisha sala mpaka saa za mwisho; hana desturi ya kusali pamoja na Jamaa.

Jibu Langu: Mimi sijali Sheikh kukosa imani nami, bali nastaa jabia sana uwongo na uzushi wake na dhana zake mbaya za hali ya juu. Mungu Mkarimu, Uhurumie umati huu ambao viongozi, waongozi na wasimamizi wake ndio masheikh wa aina hii. Sasa wasomaji wafikirie upinzani aliota Sheikh kwa ubahili na husuda yake nyingi. Ni dhahiri kwamba mimi nilikaa Aligarh kwa siku chache tu nikiwa msafiri, na ruhusa walizotolewa wasafiri na sheria ya Kiislamu kuzikataa daima ni njia ya kikafiri. Nilikuwa sina budi kuyaangalia mambo hayo yote. Basi nilifanya niliyopaswa kuyafanya. Nami siwezi kukataa kwamba katika siku hizo chache nilizokaa hapo, wakati mwengine nilikusanya sala mbili kulingana na Suna ya Mtume s.a.w., na pengine katika saa za mwisho za Adhuhuri nilisali sala zote mbili za Adhuhuri na Alasiri kwa kuzikusanya. Basi mabwana wanaojidai kumwamini Mungu Mmoja, mara moja moja wanatali nyumbani pia kwa kukusanya sala, na wanaendelea kufuata Hadithi ya kukusanya sala *bila safari wala mvua*.

Siwezi pia kukataa kwamba katika siku hizo chache sikuhudhuria kila mara misikitini. Lakini juu ya kuugua na kuwa msafiri sikuacha kabisa kuhudhuria.

Na pengine Sheikh anajua kwamba niliwahi kusali sala ya Ijumaa nyuma yake lakini sasa nina shaka imepata kusalika barabara.

Hii ni kweli, tena kweli kabisa, kwamba mimi huwa sipendi kuhudhuria misikitini katika safari. Lakini, Mungu Apishe mbali, sababu yake si uzembe au kupuuza maagizo ya Mwenyezi Mungu. Bali sababu ya kweli ni kwamba katika zama hizi, hali ya misikiti mingi ya nchi yetu ni mbovu mno na ya kusikitisha sana. Kama mtu akiendea misikiti hiyo na kutaka kuongoza katika sala, hapo maimamu wa misikiti hiyo wanakasirika mno na kughadhibika sana; na akisali nyuma yao, nina shaka kwamba sala imesalika kweli! Kwani inathibitika kwa uwazi kwamba hao wamefanya uimamu kuwa ajira nao, hawaendi mara tano kusali. Bali ni duka ambalo wanakwenda kulifungua katika nyakati hizo, na hulitegemea duka hilo kwa kupata riziki yao na ya watoto wao. Hivyo mmoja kuondolewa katika ajira hiyo na kupewa mwingine husababisha kufungua mashtaka mahakamani, na Masheikh kwa ajili ya kupigania uimamu hukata rufaa baada ya rufaa. Basi huu sio uimamu bali ni njia ichukizayo ya ulaji wa haramu. Je, si wewe pia umenaswa katika mtego huo wa nafsi! Basi kwa nini mtu apoteze imani yake baada ya kuyaona hayo yote. Kukusanyika wanafiki misikitini kulikoeleza katika Hadith za Mtume s.a.w. kuhusu zama za mwisho ndiyo bishara inayohusikana na Masheikh hao ambao wakisimama katika mihirabu wanasoma kurani Tukufu kwa midomo lakini miyoni wanahesabu chapati. Nami sijui ni tangu lini imekatazwa kukusanya sala za Adhuhuri na Alasiri au Magharibi na Isha katika hali ya safari, na ni nani aliyetoa fatuwa ya kwamba ni haramu katika saa za mwisho. Ni la ajabu kwamba kwako wewe ni halali kula nyama ya nduguyo mfile lakini ni haramu kabisa kusali pamoja Adhuhuri na Alasiri katika hali ya safari.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ قَوْمٌ مُّرَبِّطُونَ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَكْثُرُونَ

[*Mwogopeni Mungu, enyi wenye kumwamini Mungu Mmoja, kwani mauti yapo karibu na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyaficha.*]

–Mwandishi

kwa njia nyingine bila ya kuwatuma Mitume na Manabii. Au Angeleta Utume katika zama za mwanzo tu na kukoma kwa kudumu kuleta Unabii na Utume na Wahyi. Lakini hekima kubwa ya Mwenyezi Mungu na busara haikupenda hivyo, na katika nyakati za haja yaani wakati wowote upendo wa Mungu na ibada Yake na kumcha Yeye na utakaso na mengineo yaliyo wajibu yalipoingiwa na tofauti, watakatifu wakipata wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu waliendelea kufika duniani kama mifano. Na mambo yote haya mawili yanategemeana kwamba kama Mwenyezi Mungu daima Anataka kuwarekebisha viumbe, basi ni lazima pia kwamba sikuzote waendelee kufika watu ambao Mwenyezi Mungu Amewajaalia busara kutoka Kwake na kuwaimarisha katika njia a matakwa Yake. Bila shaka jambo hili ni la yakini kabisa na ni mionganoni mwa mambo yaliyokubaliwa kwamba mpango huu mkubwa wa kuwarekebisha viumbe hauwezi kutekelezwa kwa kupelekeana barua tu. Kwa shabaha hii ni lazimu kukanyaga njia ambayo Manabii watakatifu wa Mwenyezi Mungu waliendelea kuikanyaga tangu zamani. Na Islam ilipoanza tu ikaiendeleza njia hii yenye kuathiri kwa imara na uthabiti hata kwamba mfano wake haupatikani katika dini nyingine. Nani awezaye kuonyesha mahala pengine Jumuiya kubwa kama hii ambayo idadi ya wafuasi wake ilipita hata elfu kumi ambao usiku na mchana wakashinda kizingitini pa Mtume s.a.w. kwa imani kamili na unyenyekevu na juhudhi na makini kabisa kwa kupata ukweli na kujifunza huo. Bila shaka Hadhrat Musa a.s. pia alipewa Jumuiya, lakini jinsi walivyokuwa waasi, wakorofi na mbali na usahibu wa kiroho na ukweli, ni jambo wanadolielewa

vema wasomaji wa Biblia na wenye kujua historia ya Mayahudi. Lakini Jumuiya ya Mtume s.a.w. ikawa na umoja wa kiroho katika njia ya Mtume wao kwamba kwa sababu ya udugu wa Kiislamu wakawa kama kiungo kimoja kwelikweli na nuru za unabii zikapenya sana katika hali yao ya kutendeana wao kwa wao na katika maisha yao na katika hali yao ya nje na ndani kana kwamba wote walikuwa ni picha hasa za Mtume s.a.w. Basi mwujiza huu mkubwa wa mabadiliko ya ndani ambayo kwayo wenye kufanya ibada mbovu ya masanamu wakawa wenye kumwabudu Mungu kikamilifu, na waliokuwa wamezama sikuzote katika dunia, wakaungana na Mpenzi wao wa kweli hata kwamba wakamwaga damu yao kama maji katika njia Yake. Haya kwa hakika yalikuwa ni matokeo ya kuishi kwa uaminifu pamoja na Nabii mkweli na mkamilifu. Na kwa sababu hiyo nimetumwa kuja kuendeleza mpango huu na ninapenda kwamba desturi ya watu kukaa pamoja nami ipanuliwe zaidi na watu wenye shauku ya kukuza imani na mapenzi na yakini wakae nami usiku na mchana na wakadhihirikiwe nuru zilizodhihirika kwangu na wajaaliwe ladha niliyojaaliwa mimi ili nuru ya Islam itapakae duniani kote na doa jeusi la dharau na dhila liondolewe kwenye paji la uso la Waislamu. Kwa kunipatia bishara hiyo Mwenyezi Mungu Amenituma na Akasema: Ufurahi! Kwani wakati wako umekurubia na miguu ya Waislamu imeimarika juu ya mnara mrefu sana.

Tawi la nne la mpango huu ni zile barua wanazoandikiwa watafutao ukweli au wapinzani. Na hadi sasa katika muda

uliotajwa nyuma pengine barua zaidi ya elfu tisini ziliwasili ambazo zilijibowi isipokuwa baadhi ya barua zilizoonekana za kipuuzi au si za muhimu. Na kazi hii inaendelea kama kawaida na kila mwezi barua mia tatu hadi mia saba au mpaka elfu hupokelewa na kutumwa.

Tawi la tano la Mpango huu ambao Mwenyezi Mungu Ameuanzisha kwa wahyi na ufunuo Wake maalum ni kufika mfululizo wafuasi na wafanyao baiati. Basi wakati wa kuanzisha Jumuiya hii Yeye Aliniambia: Ardhi imepigwa na tufani ya upotevu. Tayarisha safina hii katika wakati huu wa tufani; yule atakayepanda safina hii ataokoka asighariki, na atakayekataa atayakabili mauti. Na akasema: Awekaye mkono wake juu ya mkono wako, haweki mkono wake juu ya mkono wako, bali auweka juu ya mkono wa Mwenyezi Mungu. Na Mungu Huyo Akanipa bishara kwamba: Nitakufisha na kukunyanya Kwangu, lakini wafuasi wako na wapenzi wako wa kweli wataendelea kuwepo hadi siku ya Kiyama na daima watakuwa na ushindi juu ya wakataaji.

Hizo ni aina tano za mpango ambao Mwenyezi Mungu Ameuanzisha kwa mkono Wake Mwenyewe. Ingawa mwenye kuangalia juu juu ataona kazi ya kutunga vitabu tu ndiyo kitu cha lazima na matawi mengine si ya lazima wala ya maana. Lakini mbele ya Mwenyezi Mungu hayo yote ni ya lazima, na marekebisho Aliyoyakusudia hayawezekani bila kutumia njia hizo tano. Ingawa mpango wote huu unategemea msaada na fadhili maalum za Mwenyezi Mungu na Yeye Mwenyewe Anatosha kuufanikisha, na

ahadi Zake zenyе bishara zinatutuliza, lakini kwa sababu ya Yeye kuamuru na kuhimiza, Waislamu wanaelekezwa kutoa msaada kama Manabii wote wa Mwenyezi Mungu waliopita walivyoendelea kuhimiza wakati wa shida. Basi kwa kuelekeza huko ninasema kwamba ni dhahiri ya kuwa kuendelea kwa matawi hayo matano kuna njia bora na pana, msaada mwangi kiasi gani wa Waislamu kwa jumla unahitajika. Kwa mfano, zingatieni mpango wa utungaji wa vitabu tu kwamba kama tukichukua jukumu la huduma kwa shabaha ya kuvieneza sawasawa, tutahitaji mali nyingi kiasi gani kuikamilisha. Kwani kama kweli shabaha yetu ni kukamilisha uenezaji, basi kusudio letu liwe kwamba viatbu vyetu vya kidini ambavyo vimejaa johari za utafiti na uchunguzi, na vyenye kuwavutia watafutao ukweli kwenye njia iliyo sawa, viwafikie haraka sana tena kwa wingi watu ambao kwa kuathirika na mafundisho mabovu wameugua maradhi ya kuangamiza au wamekwisha kurubia mauti. Na wakati wote tuzingatie kwamba nchi ambayo imo hatarini kwa sababu ya sumu iuayo ya upotevu, vitabu vyetu vienee nchini humu haraka sana na vitabu hivyo vifikie mkononi mwa kila mtafuta ukweli. Lakini ni dhahiri kwamba kupata hiyo kikamilifu na kitimilifu haiwezekani kushikilia sikuzote kwamba vitabu vyetu viendelee kuenea kwa njia ya kuuzwa. Kuvichapa vitabu kwa shabaha ya kuviuza na kuingiza dini ndani ya dunia kwa sababu ya kuingiwa na tamaa ya nafsi ni njia mbovu sana na ya kulaumiwa ambayo kwa nuksi yake hatuwezi kueneza haraka vitabu vyetu duniani wala hatuwezi kuwapatia watu vitabu hivyo kwa wingi. Bila shaka jambo hili ni kweli kabisa kwamba kwa mfano kama

tukigawa bure vitabu laki moja, tunaweza kuvifikisha vitabu vyote hivyo kwenye nchi za mbali katika siku ishirini tu na twaweza kuvieneza kwa jumla katika madhehebu yote na mahali pote na kumpa kila mtafuta haki na ukweli. Kazi kama hiyo ilio nzuri mno hatutaweza kuitekeleza pengine katika muda wa miaka ishirini. Tukiiza vitabu tutapaswa kuviweka masandukuni na kuwangojea wanunuzi kwamba lini anakuja ye yote au anatuma barua (ya kuagiza). Na inawezekana katika muda huo mrefu wa kungojea sisi wenyewe tuage dunia hii na vitabu vikabakia masandukuni. Basi kwa kuwa eneo la uu zaji vitabu ni dogo sana na ni kikwazo kikubwa cha kupata shabaha hasa, na kazi ya miaka michache itafanyika katika mamia ya miaka na hadi sasa mionganoni mwa Waislamu tajiri ye yote mwenye moyo mkunjufu na mkarimu hakuelekea kununua nakala nyingi sana za vitabu vyetu vipya na kuzigawa kwa ajili ya Mungu tu; na katika Islam hakuna chama kama misheni za Kikristo kinachoweza kusaidia katika kazi hii;¹⁰ na maisha pia hayategemewi ili kutumai kupata umri mrefu tuendelee kungojea kwa muda mrefu sana; kwa hivyo, tangu mwanzo nimejiwekea utaratibu huu

¹⁰ Inaelezwa kwamba British and Foreign Bible Society tangu ianze yaani katika muda wa miaka ishirini na mmoja iliyopita imeeneza kwa kugawa duniani vitabu vyake zaidi ya milioni sabini kuhakikisha ukweli wa dini ya Kikristo. Waislamu wa zama hizi walio na uwezo lakini ni wazembe wanapaswa kusoma kwa uangalifu na kwa kuona haya makala iliyochapwa na kuenezwa katika magazeti ya Oktoba na Novemba mwaka 1890. Je, vitabu hivyo vimeenezwa na wauzaji? Au vimetolewa bure na jamii ya watu wenye bidii kwa kusaidia dini yao? (Mwandishi)

kuhusu vitabu vyangu vyote kwamba, iwezekanavyo, vitabu vingi zaidi vitolewe bure ili vitabu hivyo vilivyojaa nuru ya ukweli kwa jumla vienee haraka sana duniani. Lakini kwa kuwa mimi binafsi nilikuwa sina uwezo wa kubeba mzigo huu mkubwa peke yangu na pamoja na hayo kulikuwa na matumizi makubwa ya matawi mengine pia, hivyo kazi hii ya uchapishaji vitabu ilisimama baada ya kuendelea kwa muda fulani, ambayo bado imesimama mpaka leo. Mbele ya Mwenyezi Mungu matawi yote ya Mpango huu ni ya namna moja na Yeye Anataka yote hayo yakamilike na kustawi kwa usawa. Lakini matumizi ya matawi hayo matano yako mengi kwamba yanahitaji maelekeo maalum na huruma ya wenyewe iklasi. Kama nikiandika maelezo kamili ya matumizi hayo ya kidini, yatakuwa marefu sana. Lakini enyi ndugu, zingatieni, kwa mfano, wanaokuja na kuondoka; hadi sasa katika muda wa miaka saba, wageni karibu elfu sitini au zaidi wamekuja. Sasa mwaweza kukisia kwamba kwa kuwahudumia na kuwakirimu wageni hao wapenzi gharama kiasi gani zilitumika, na kwa raha yao katika majira ya baridi na joto vifaa gani vililazimika kuwekwa tayari. Bila shaka mtu mwenye busara atastaajabu kwamba mahitaji na hatua mbali mbali za kuwakirimu wageni wengi namna hii ziliwezaje kutekelezwa mara kwa mara na kazi kubwa kama hiyo inaendeleaje bado? Kadhalika matangazo elfu ishirini yaliyochapwa kwa Kiingereza na Kiurdu na zaidi ya elfu kumi na mbili yalitumwa kwa rejista kwa viongozi wapinzani. Na hamna padre hata mmoja nchini India asiyeperekewa matangazo hayo bali kwa kutumwa matangazo hayo kwenye nchi za Ulaya na Amerika kwa rejista, hoja ilikamilishwa. Je,

si jambo la ajabu kwamba fedha hizi kidogo zinatoshelezaje matumizi hayo, na hayo ndiyo matumizi yaliyo makubwa zaidi. Lakini kama zikiangaliwa gharama zinazotumika kutuma barua kila mwezi, hizo pia ni fedha nyingi ambazo kuziendeleza hizo mpaka sasa hakuna njia ya kupata msaada.

Na wale ambao baada ya kujiunga na jumuiya, wanapenda kukaa kwangu wakitafuta ukweli kama watu wa Suffa, naangalia upande wa mbinguni kwa matumizi yao pia. Nami najua kwamba kwa kudumisha matawi haya matano Mungu Mweza Mwenyewe Ataleta njia Ambaye kwa matakwa yake msingi wa mpango huu umewekwa, lakini kwa shabaha ya mahubiri ni lazima kuwajulisha watu habari hii. Nimesikia kwamba baadhi ya watu wasiofahamu wananaillaumu kwamba nilichukua toka kwa watu bei ya kitabu cha Barahine Ahmadiyya na pia michango kiasi fulani rupia elfu tatu takriban, lakini hadi sasa kitabu hakijachapwa kikamilifu. Nikijibu nawaambia kwamba rupia zilizopokelewa kutoka kwa watu siyo elfu tatu tu, bali zaidi ya hizo rupia nyingine pia elfu kumi takriban ziliuja ambazo hazikutolewa kama mchango wa kitabu hicho wala si kama bei yake, bali baadhi ya watu walioomba waombewe dua walizitoa hizo kama zawadi, au baadhi ya marafiki walizitoa kwa upendo wao; basi zote hizo ziliendelea kutumika mara kwa mara kutekeleza shughuli za muhimu na kazi nyingine za mpango huu. Na kwa kuwa hekima ya Mungu iliahirisha mpango wa utungaji wa kitabu, ndiyo sababu hakikubakia kitu kwa ajili yake baada ya kugharamia matawi mengine muhimu yaliyoanzishwa kwa amri ya Mungu. Na hekima iliyomo katika kuahirika

uchapishaji wa kitabu hicho ndiyo hii kwamba katika kipindi cha muda huo baadhi ya mambo mepesi na ya ukweli yapate kufunguka kikamilifu kwa mwandishi na wapinzani watoe harara yao yote. Sasa Mungu Alipotaka tena kwamba vitabu vilvyobakia vikamilike kutungwa, Akanielekeza kuandika madhumuni ya mwito huu. Basi wakati huu, nahitaji sana kukamilisha utungaji wa vitabu. Sehemu kubwa ya Barahine-Ahmadiyya bado inahitaji kuchapishwa. Kama ikiwa tayari basi wapelekwe wanunuzi na wale wote waliopatiwa sehemu za kwanza lilahi tu, na wakaahidiwa kupewa baadaye pia. Hali kadhalika nataka kuandika vitabu vingine kama vile Ashi‘atul Kuran, Siraj-e-Munir, Tajdid-e-Din, Arbain fi alamatil Mukarrabin na maelezo ya Kurani Tukufu. Na pia nina jazba moyoni kwamba kwa kubatilisha dini batili kama vile Ukristo na kuyakabili magazeti yao lichapishwe jarida moja la kila mwezi. Na ili kuendeleza mfululizo kazi hizo zote hakuna kizuizi katikati isipokuwa mtaji na msaada wa kifedha. Kama tupate mtambo wetu wa uchapishaji na tuwe na mwandishi mmoja akae kwetu sikuzote kwa kudumu, na tuwe na uwezo wa kugharamia gharma zote za lazima, yaani gharama zote za karatasi na uchapishaji na mishahara ya waandishi tuendelee kupata mara kwa mara, hapo mpango wa kutosha utafanyika wa kukuza tawi moja katika matawi haya matano.

Ewe nchi ya India! Je ndani yako hamna tajiri ye yote mwenye uwezo ambaye kama si zaidi basi kwa akali aweze kubeba gharama ya tawi hili peke yake?

Kama waaminio watano wenye uwezo wautambue wakati

huu, basi wanaweza kujibebea majukumu ya kuyasimamia matawi haya matano, kila mmoja tawi moja moja. Ewe Mungu Mweza, izindue miyo hii Wewe Mwenyewe. Islam bado haijawa maskini kiasi hiki; ni moyo tu mdogo, sio umaskini. Na watu wasio na uwezo kamili nao wanaweza kuusaidia mpango huu kwa kuutolea fedha kidogo kidogo kama msaada wa kila mwezi sawa na uwezo wao kwa ahadi imara. Kamwe haifaidiki dini na uzembe, kutojali na dhana mbaya. Dhana mbaya huzifanya nyumba ziwe kiwa na kuleta mafarakano nyoyoni. Tazameni, waliopata zama za manabii, walijitahidi namna gani kueneza dini. Jinsi alivyotoa tajiri mali yake aipendayo katika njia ya dini, ndivyo alivyoleta maskini hohehahe mfuko wake uliojaa makombo aliyopenda, na wakadumu kufanya hivi mpaka ukaja wakati wa ushindi toka kwa Mwenyezi Mungu. Si rahisi kuwa Mwislamu, si sahihi kupata lakabu ya mumini. Basi enyi watu! Kama mnayo roho ya ukweli wanayojaaliwa waaminio, msiuchukulie mwito wangu huu kijuujuu. Tafuteni kupata wema, kwani Mwenyezi Mungu Anawaangalieni huko mbinguni mnaukitikiae ujumbe huu.

Enye waislamu mliongwa athari zilizobakia za waaminio wenye azma na dhuria ya watu wema, msiharakie kukataa na kuwa na dhana mbaya, na yaogopeni maradhi ya kutisha ya kuambukiza yanayoenea pembezoni mwenu, na watu wasiohesabika wameisha naswa katika mtego wake wa ulaghai. Mwaona jinsi inavyotiliwa bidii kwa nguvu sana kuifutilia mbali dini ya Kiislam. Je haiwalazimuni nyinyi nanyi mjibidiishe? Islam haikutoka kwa binadamu ili iweze kuangamia kwa juhudini za kibinadamu. Lakini ni masikitiko

kwa wale wanaokusudia kuing'olea mbali; tena masikitiko mengine ni kwa wale ambao wana kila kitu kwa anasa za wake zao, watoto wao na nafsi zao, lakini hamna mifukoni mwao kitu kwa ajili ya Islam. Ole wenu, enyi wazembe! Nyinyi hamna uwezo wowote wa kuishindisha Islam na kuonyesha nuru za dini, lakini hamwezi hata kuupokea kwa shukrani mpango ulioanzishwa na Mwenyezi Mungu kwa kudhihirisha mng'ao wa Islam. Siku hizi Islam ni kama taa ifungiwayo sandukuni au ni kama chemchem tamu ifichwayo na takataka. Ndiyo sababu Islam imerudi nyuma, uso wake mzuri hauoneki, umbo lake la kuvutia halionekani. Ilikuwa ni faradhi ya Waislamu kufanya juhudi kwa kuonyesha sura yake ipendwayo. Na si mali tu bali wangemwaga damu pia kama maji, lakini hawakufanya hivyo. Kwa ujinga wao wa hali ya juu wamenaswa katika kosa hili kwamba je vitabu vya zamani havitoshi? Hawajui kwamba kwa kuuondoa ufisadi wa kisasa ambao unaendelea kudhihirika kwa sura mpya mpya, yalazimu kinga yake pia nayo iwe ya kisasa. Tena katika wakati wa kutapaka giza la kila zama manabii, mitume na wasuluhishi waliendelea kufika, je havikuwepo vitabu vilivyotangulia wakati huo? Basi enyi ndugu! Wakati giza lieneapo, ni lazima nuru iteremke toka mbinguni.

Nimekwisha eleza katika makala haya kwamba Mwenyezi Mungu ndani ya sura Al-Qadr Anawapasha waaminio habari njema kwamba maneno yake na nabii wake ametermshwa toka mbinguni ndani ya Lailatul Kadr. Na kila msuluhishaji na mujaddidi ajaye toka kwa Mwenyezi Mungu huteremka tu katika Lailatul Kadr. Je, mnafahmu kwamba Lailatul Kadr ni kitu gani? Lailatul Kadr ni zama zile za giza ambazo giza

lake linafikia upeo wa mwisho kabisa. Kwa hiyo, zama hizo kitabia zinataka nuru fulani iteremke kuliondoa giza hilo. Zama hizo, kwa njia ya istiara zaitwa Lailatul kadr. Lakini kwa hakika huo sio usiku, bali ni zama ambazo kwa sababu ya giza zimefanana na usiku. Baada ya kifo cha nabii au cha khalifa wake, miezi elfu moja inapopita, ambayo inasogeza umri wa mtu karibu na mwisho, na kutoa habari ya hisia za kibinadamu kutoweka, ndipo usiku huu huanza kutawala. Basi hapo ndipo kwa mpango wa kimbunguni hupandwa kwa kisiri mbegu ya msuluuhishi mmoja au wengi, ambao hutayarishwa ndani kwa ndani kwa kudhihiri mwanzoni mwa karne mpya. Kwenye habari hiyo Mwenyezi Mungu Anaashiria kwa kusema:

نَٰيْلَةُ الْقَدْرِ حَيْثُ مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ^{١١}

Yaani aionaye nuru ya Lailatul Kadr hii na kupata heshima ya kukaa pamoja na msuluuhishi wa zama, ni bora kuliko mzee wa miaka themanini asiyeupata wakati huu wenye nuru. Na kama aupate wakati huo hata kwa muda kidogo, huo muda ni bora kuliko hiyo miezi elfu moja ilyopita awali. Ni bora kwa nini? Kwa sababu katika Lailatul Kadr hiyo Malaika wa Mwenyezi Mungu na Ruhul Kudus (Jibrili) pamoja na msuluuhishaji huyo huteremka toka mbinguni kwa idhini ya Mungu Mwenye Jalali, si bure tu bali ili waziteremkie nyoyo zilizo tayari kukubali ukweli, na kufungua njia za usalama. Basi wao hushughulikia kufungua njia zote na kuyaondoa mapazia yote hata kwamba giza la kughaflika likiondoka

¹¹ Al-Qadr, 97:4

asubuhi ya mwongozo hudhihirika.

Sasa enyi Waislamu, zisomeniaya hizo kwa makini, mkaone jinsi Anavyozisifu Mwenyezi Mungu zama hizi, ambamo Humtuma msuluhishaji duniani katika wakati wa haja. Je, hamtathamini zama hizo? Je, mtazichukulia kauli za Mwenyezi Mungu kimasihara?

Basi enyi Waislamu wenyewe uwezo, angalieni! Mimi ninawafikishieni ujumbe huu kwamba mnapaswa kuusaidia mpango huu wa kusuluuhisha, uliotoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa moyo wenu wote na mwelekeo wenu wote na ikhlasi yenu yote na kuziangalia jiha zake zote kwa hesima mwutolee huduma haraka sana. Yule anayetaka kutoa chochote kila mwezi sawa na uwezo wake na atoe mwenyewe kila mwezi kuifikiria kuwa ni wajibu na deni la lazima. Na akiisha ufanya wajibu huu kuwa nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu asihalifu wala kupuza kuitimiliza. Na atakaye kutoa kama msaada mara moja kwa mpigo na atoe hivyo. Lakini izingatiwe kuwa shabaha hasa ambayo kwayo mpango huu unatumaniwa kuendelea bila kukatika ni utaratibu huu ya kuwa waitakiao heri dini kikweli wafunge ahadi madhubuti ya kutoa fedha, kwa suhula kila mwezi sawa na uwezo na wasaa wao, ambazo waweza kuzitoa bila shida sharti kusipatikane na kizingiti. Naam, yule ambaye Mwenyezi Mungu amemjaalia utulivu wa moyo, ye ye mbali na mchango wa kila mwezi anaweza kutoa msaada wa utoaji wa mpigo sawa na uwezo na wasaa wake.

Na nyinyi enyi mahabubu zangu, matawi mabichi ya mti wa dhati yangu, ambao kwa rehema za Mwenyezi Mungu zilizo

juu yenu mmeingia katika silsila ya baiati yangu na mnatoa muhanga uhai wenu, raha zenu na mali zenu katika njia hii, ingawa ninafahamu kuwa nitakalosema mtaona ni bahati mzuri kulikubali na hamtasita kutoa kadri ya uwezo wenu, lakini siwezi kuwawekeeni faradhi ya kutoa kiasi maalum kwa huduma hii kwa ulimi wangu, ili huduma zenu zisiwe zimelazimika kwa usemi wangu bali ziwe kwa furaha yenu wenyewe.

Rafiki yangu ni nani? Na mpendwa wangu ni nani? Ni yule tu anayenitambua. Ni nani anayenitambua? Ni yule tu aliye na yakini nami kuwa nimetumwa, naye ananikubali kama wanavyokubaliwa wanaotumwa. Dunia haiwezi kunikubali, kwani sitokani na dunia hii. Lakini wale ambao tabia yao imejaaliwa sehemu ya ulimwengu ule, ndio wanankubali na watanikubali. Yule anayeniacha ndiye anayemwacha Yule Aliyenitura; na yule anayeungana nami ndiye anayeungana na Yule Ambaye mimi nimetoka kwake. Mkononi mwangu mna taa, ajaye kwangu ni lazima atapata sehemu ya nuru hii. Lakini anayenikimbia kwa sababu ya wasiwasni na dhana mbaya, atatupwa gizani. Mimi ndimi ngome madhubuti ya zama hizi; anayeingia kwangu atajio koa uhai wake dhidi ya wezi, majambazi na wanyama mbuai. Lakini anayetaka kukaa mbali na kuta zangu, huyo kutoka kila upande anakabiliana na mauti na maiti yake pia haitakuwa salama. Ni nani aingiaye ndani mwangu? Ni yule tu aachaye maovu na kushika wema, na kuacha upotovu na kupiga hatua kwenye uongofu na kuwa huru katika utumwa wa shetani na kuwa mja mtiifu wa Mwenyezi Mungu. Kila afanyaye hivyo yumo ndani mwangu, nami nimo ndani mwake. Lakini yule tu ana uwezo wa

kufanya hivyo ambaye Mwenyezi Mungu Anamweka katika kivuli cha mtu mwenye nafsi itakasayo. Ndipo huyo aweka mguu wake katika moto wa nafsi yake basi hapo inapoa nafsi hiyo kabisa, kana kwamba humo hamkuwahi kuwa na moto hata kidogo. Hapo hupata maendeleo juu ya maendeleo hata kwamba Roho ya Mwenyezi Mungu hukaa ndani yake, na kwa mdhihiriko makhsus wa Mola wa walimwengu hustawi juu ya moyo wake. Ndipo utu wake wa zamani ukiungua na hupewa utu mpya uliotakasika, na Mwenyezi Mungu pia akiwa Mungu mpya Hushika naye uhusiano mpya, na katika ulimwengu huu huu anapatiwa mahitaji yote matakatifu ya maisha ya Peponi.

Hapa sina budi kueleza jambo hili na kumtolea shukrani Mwenyezi Mungu kwamba Yeye kwa fadhili na ukarimu Wake Hakuniacha mpweke. Wanaofungamana nami kidugu na kuingia katika Jumuiya hii ambayo Mwenyezi Mungu ameianzisha kwa mkono Wake, wamejazwa kiajabu upendo na ikhlasi; na si kwa juhudini yangu bali Mwenyezi Mungu kwa hisani yake makhsus Alinipatia roho hizi zilizojaa ukweli. Kwanza kabisa ninacho kiherehere moyoni mwangu cha kumtaja ndugu yangu mmoja wa kiroho, anayeitwa jina Nurdin sawa na nuru ya ikhlasi yake. Mimi daima namtazama kwa macho ya kumwonea wivu kutokana na baadhi ya huduma zake za kidini anazofanya kwa kutumia mali yake ya halali, kwa ajili ya kushindisha neno la Islam, kwamba laiti huduma hizo zingeweza kufanywa nami pia. Kwa kuwaza jazba ya kuisaidia dini iliyojaa moyoni mwake, taswira ya uwezo wa Mwenyezi Mungu inakuja mbele ya macho yangu, kwamba Anawavutiaje waja wake kwake. Yeye kwa mali zake zote na

nguvu yake yote na uwezo wake wote alio nao, kila wakati amejiweka tayari kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Nami kutokana na uzoefu, si kwa dhana njema tu, ninayo elemu sahihi na ya kweli kwamba ye ye hajali katika njia yangu, si mali tu bali hata uhai wake na heshima yake. Na kama ningemruhusu, basi kwa kutoa kila kitu katika njia hii angetimiza haki ya kukaa nami daima kwa kiwiliwili jinsi alivyokaa nami kiroho. Naandika hapa mistari michache ya baadhi ya barua zake kama mfano ili wasomaji wafahamu kwamba ndugu yangu mpendwa Maulawii Hakim Nuruddin wa Bhera, tabibu wa serekali ya Jammu, ameendeleaje mbele sana katika madaraja ya upendo na ikhlasi. Na mistari yenewe ndiyo hii:- Maulana, Mwongozi wetu, Imam wetu, Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu.

Mheshimiwa, naomba dua kwamba saa zote niwe pamoja nawe, nikapate kutoka kwa Imamu wa zama matilaba ambayo kwayo amefanywa kuwa Mujaddidi. Kama ningeruhusiwa, ningojiuzulu kazi na ningeshinda kwako usiku na mchana. Au kama nikiamriwa niondoke na kuzunguka duniani kote na kuwaita watu kwenye dini ya haki na kufia katika njia hii. Nimejitolea kwako. Chochote nilicho nacho si changu, ni chako. Mheshimiwa Mwongozi wangu, nasema kwa kweli kabisa kuwa ikiwa mali yangu yote itumike katika kueneza dini, nitapata shabaha yangu. Kama wale waliota mapema bei ya kukinunua Barahin wana wasiwasi kwa kuchelewa kwa uchapishaji wa kitabu, basi niruhusu mimi nitoe huduma hii ndogo ya kuwarudishia bei yao yote waliyokwisha toa. Mheshimiwa mwongozi wangu! Mimi niliye mzembe na mnyenyekemu nasema, ukikubali nitakuwa na bahati njema,

kwamba ningependa gharma zote za uchapishaji wa Barahin ziwejuu yangu, na kiasi chochote kitakachopatikana kwa mauzo yake, fedha hizo zitumike kwa mahitaji yako. Nina uhusiana na wewe Kifaruki, (kama Seyyidna Umar Faruk alivyohusiana na Mtume s.a.w) niko tayari kutoa kila kitu katika njia hii, niombee mauti yangu yawe mauti ya Masiddiki.

Uaminifu na bidii ya Maulawii Sahib msifika na huruma yake na kujitolea kwake, kama inavyodhahirika kwa kauli yake, ndivyo inavyodhahirika kwa wingi zaidi kwa hali yake na kwa huduma zake zenye ikhlasi. Na kwa mahaba na jazba kamili ya ikhlasi anapenda atoe mhanga katika njia hii kila kitu hata vitu vya lazima vya matumizi ya watoto wake pia. Roho yake na jazba ya upendo inamhimiza kupiga hatua mbele zaidi ya uwezo wake na anashughulikia kuhudumia kila saa na kila wakati.¹²

Lakini itakuwa ni dhuluma kubwa kumtwisha mwenye kujitolea muhanga mizigo yote zaidi ya uwezo wake, ambayo kuibeba ni kazi ya kundi la watu. Hamna shaka

¹² Hadhrat Maulawii Sahib ana ujuzi wa kiwango cha juu katika elimu ya Fik'hi, Hadithi na maelezo ya Kurani. Ana ufahamu mkubwa sana wa Falsafa na Sayansi za kale na za kisasa. Katika fani ya utabibu yu tabibu mahiri. Ameandaa maktaba isiyo kifani kwa kuagiza vitabu vya kila fani toka nchi za Misri, Uarabu, Shamu na Ulaya. Na kama vile alivyo mwanachuoni mkubwa katika elimu nyingine ndivyo alivyo na busara kubwa ya mijadala ya kidini. Ni mwandishi wa vitabu bora kabisa. Hivi majuzi kitabu cha «*Tasdiki Barahine Ahmadiyya*» pia alikitunga Mheshimiwa Msifika, ambacho kina thamani nyingi zaidi kuliko johari machoni mwa kila mtu mwenye tabia ya kufanya utafiti. (Mwandishi).

katika kutoa huduma hii, Maulawii Sahib atakubali kutoa mali yake yote na kusema kama Nabii Ayubu a.s alivyosema kwamba “nilikuja peke yangu na nitaondoka peke yangu”.¹³ Lakini faradhi hii ni ya watu wote, na wote wanalazimika kwamba katika zama hizi zilizojaa hatari na fitina, ambazo zinatikisisha kwa kishindo uhusiano mwororo wa imani unaostahili kuwepo kati ya Mwenyezi Mungu na mja wake, wafikirie mwisho wao mwema, na kutenda amali njema zilizo chanzo cha wakovu kwa kutoa mali zao wanazopenda na kutumia nyakati zao wanazothamini, na mwogope kanuni ya Mwenyezi Mungu isiyobadilika na iliyo imara aliyoeleza katika maneno yake matakatifu:

لَنْ تَأْتُوا إِلَيْنَا حُلُّ شَفَاعَةٍ مَّا نَجَّبُونَ¹⁴

Yaani, hamwezi kamwe kuufikia wema wa kweli unaofikisha hadi wokovu mpaka mtoe katika njia ya Mwenyezi Mungu ile mali na vile vitu mnavyopenda. Hapa naona inafaa kuwataja marafiki zangu wapenzi wengine wachache ambao wamo katika Jumuiya hii ya Mungu nao wanipenda sana kwa moyo wote. Mionganini mwa ni ndugu yangu Sheikh Muhammad Husain wa Muradabad, ambaye akiwasili Qadian wakati huu kutoka Muradabad, anaendelea kunukuu maandishi haya kwa kuchapishwa kwa kupata radhi ya Mwenyezi Mungu.

¹³ Katika maana hii kitabu cha Ayubu kinasema “Akasema mimi nilitoka tumboni mwa mama yangu nili uchi, nami nitarudi tena huko uchi vile; Bawana alitoa, na Bwana ametwaa.”

¹⁴ Ayubu, 1:21

Aali-‘Imran, 3:93

Moyo safi wa Bwana Sheikh msifiwa nauona kama kioo. Ananipenda kwa ikhlasi na mahaba ya daraja la juu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Moyo wake umejaa mapenzi kwa Mwenyezi Mungu. Yu mtu wa ajabu sana. Namwona yu taa ing'aayo kwa ajili ya Muradabad; natumaini kwamba ile nuru ya upendo na ikhlasi aliyo nayo, siku moja itawapenya wengine pia. Ingawa Bwana Sheikh ni mwenye uwezo mdogo, lakini ni mkarimu na ana moyo mkunjufu. Anashughulikia kunihudumia kwa kila namna. Imani yake iliyojaa upendo imenyoweshwa mishipani mwake.

Rafiki mwingine ni ndugu Hakim Fadhl Din wa Bhera. Bwana Hakim msifiwa, kiasi alicho nacho kwangu upendo, ikhlasi, itikadi njema na uhusiano wa ndani, nashindwa kueleza. Yu mwanamume mwenye kunitakia mema kikweli, kunihurumia kwa moyo na mwenye kutambua ukweli wa mambo. Baada ya Mwenyezi Mungu kunielekeza kuandika kijitabu hiki na kunipa matumaini kwa funuo zake makhsus, niliwaeleza watu kadha kukiandika kijitabu hiki, lakini hakuna yejote aliyeafikiana nami. Lakini ndugu yangu mpenzi, pasipo mimi kumwambia, akanihamasishia mwenyewe kuandika kitabu hiki na akatoa rupia mia moja kwa ajili ya kukigharamia. Nastaajabia busara yake ya kiimani kwamba dhamira yake imeenda sambamba na dhamira ya Mwenyezi Mungu. Daima hutoa huduma kwa siri, na amekwisha toa rupia mia kadha kwa siri katika njia hii, kwa ajili tu ya kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu na ampatie malipo mema.

Miongoni mwao kuna ndugu yangu mpenzi sana

aliyetuhuzunisha kwa kutuaga, Marehemu Mirza Adhim Beg, Mtemi wa Samana, eneo la Patiala, alifariki dunia tarehe mbili ya mwezi wa Rabii II, mwaka 1308 hijria.

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِحُونَ - الْعَيْنَ تَدْمَعُ
 ١٥ وَالْقُلُبُ يَخْرُجُونَ وَإِنَّا بِفِرَاقِهِ لَمُحْزَنُونُونَ

Marehemu Mirza kadri anavyonipenda kwa ajili ya Mungu tu na kujipoteza katika upendo wangu, nilete toka wapi maneno yafaayo ya kufafanua daraja lake la kiashiki. Na kiasi cha huzuni niliyopata kutokana na kuaga kwake wakati usiotarajiwa, naona mfano wake kidogo sana katika siku zilizopita. Yeye yu mtangulizi wetu aliyetuondoka ghafla. Maadamu tuko hai kamwe hatutaisahau huzuni ya yeye kutuaga.

*Moyoni mwangu mna uchungu sana hata kwamba
 nikiweka mkono wa kanzu mbele ya machozi, hayo
 yatalilowesha hadi upindoni mwa kanzu langu.*

Kwa kukumbuka kifo chake, majonzi mnajaa moyoni na kwikwi kwa uchungu mwingi kifuani na huzuni moyoni na machozi yatiririka machoni. Dhati yake yote ilikuwa imejaa upendo. Marehemu Bwana Mirza alikuwa shujaa kweli wa kudhihirisha jazba za upendo. Alikuwa ametoa wakfu maisha yake yote katika njia hii hii. Situmai kama aliwhahi kuona kitu kingine chochote hata katika ndoto. Ingawa

¹⁵ Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Jicho latiririka machozi na moyo wahuzunika, nasi kwa kuaga kwake twahuzunika.

Bwana Mirza alikuwa ni mtu mwenye hali ndogo sana, lakini machoni mwake mali haikuwa na thamani hata kuliko vumbi kulingana na huduma za dini alizokuwa akitoa daima. Alikuwa na fahamu nzuri ya hali ya juu ya kutambua siri ya maarifa. Yakini ilijojaa mapenzi aliyokuwa nayo kunihusu mimi ilikuwa ni mwujiza wa kudra kamili ya Mwenyezi Mungu. Moyo ulikuwa unafurahi kwa kumwona, namna ulivyofurahika kwa kuona bustani ilijojaa maua na matunda. Kidhahiri amewaacha nyuma waliomtegemea, akiwemo mtoto mchanga katika hali ya udhaifu mno na umaskini bila chochote. Ewe Mwenyezi Mungu Mweza yote, Uwe Mtoshelezaji na Mlinzi wao na Uwafunulie miyoni mwa wanipendao kwamba wawahurumie ipasavyo wafiwa wa ndugu huyu mwaminifu, waliobaki bila kitu chochote.

Ee Mungu! Mfariji wa moyo wenye huzuni, Ee kimbilio la wanyonge, na Msamehevu kwa wenye dhambi! Kwa ukarimu wako msamehe sana mja wako huyo. Uwarehemu sana mno wafiwa walioachwa nyuma.

Nimewataja hapo baadhi ya marafiki kwa mfano tu na wapo marafiki zangu wengine pia wa aina na shani hii hii ambao, inshaallah, nitawaeleza kwa kirefu katika kijitabu kingine. Sasa kwa kuwa habari hii imekuwa ndefu naishia hapa.

Na hapa naona yafaa nieleze kwamba watu waliokwisha ingia ndani ya silsila yangu ya baiati, wote hao hawajastahili bado kwamba niweze kuwa na rai bora juu yao; bali baadhi

yao wanaonekana kuwa kama matawi yaliyokauka ambao Mola wangu aliye Mlinzi wangu Atawatenganisha nami na kuwatupa katika kuni.

Pia wapo wengine ambao mwanzoni walikuwa na uchungu wa moyo na ikhlasi, lakini sasa wamekunjikiwa moyo na haikubakiwa na harara ya ikhlasi na nuru ya mapenzi ya kiifuasi, bali zimebakia hila tu kama za Bal'am, na kama meno mabovu yasiyofaa kitu ila yang'olewe toka kinywani na kutupiliwa chini ya miguu. Wamechoka na kushindwa, na dunia hii mbovu imewatega katika mtego wake wa udanganifu. Basi, nasema kweli kweli kwamba karibuni watatenganishwa nami, isipokuwa yule mtu ambaye fadhili ya Mwenyezi Mungu imshike upya mkono wake. Pia wapo wengi ambao Mwenyezi Mungu amenipa kwa milele, nao ni matawi mabichi ya mti wa dhati yangu, nami wakati mwingine, inshaallah, nitaeleza habari zao.

Hapa nataka kuondoa pia wasiwasi wa baadhi ya watu ambao ni wenye uwezo na wanajidhania kuwa wakarimu sana na wenye kujitolea mhanga katika njia ya dini, lakini wanakataa katakata kutumia mali zao katika mahali pafaapo, na kusema kwamba kama tungezipata zama za mkweli aliyesaidiwa na Mungu ambaye angetoka kwa Mwenyezi Mungu kuisaidia dini, tungemkimbilia kumsaidia, hata tungejitoa mhanga, likini tufanyaje, kila mahali kuna hila na udanganyifu tu. Lakini enyi watu! Ibainike kwenu kwamba mtu mmoja ametumwa kwa kusaidia dini, lakini hamkumtambua. Yu

baina yenu na ndiye huyu anayeongea. Lakini ziko pazia nzito kwenye macho yenu. Ikiwa miyo yenu inatafuta ukweli, basi ni rahisi sana kumjaribu anayedai kuongea na Mwenyezi Mungu. Njoni kwake, kaeni pamoja naye kwa wiki mbili, tatu, ili kama Mwenyezi Mungu akipenda mjionee wenyewe mvua zile za baadhi za baraka zinazomnyeshea na nuru za wahyi wa kimbunguni zinazomteremkia. Atafutaye ndiye apataye, na agongaye ndiye afunguliwaye. Kama mkifumba macho yenu na kujificha katika chumba chenye kiza kisha mkasema kwamba jua li wapi? basi lalamiko lenu hili litakuwa ni bure tu. Ewe mjinga! Fungua mlango wa chumba chako na ondoa pazia iliyo juu ya macho yako ili si tu ulione jua bali ili likuangaze kwa nuru yake.

Wengine wanasema kwamba kuanzisha vyama na kufungua madarasa yatosha tu kuisaidia dini. Lakini hawafahamu dini ni kitu gani, na shabaha hasa za maisha yetu ni nini, na shabaha hizo zaweza kupatikana namna gani na kwa njia gani? Basi wapaswa kufahamu kuwa shabaha hasa ya maisha haya ni kupata fungamano la kweli na la yakini na Mwenyezi Mungu, ambalo hufikisha kwenye chemchem ya wokovu likituachisha na mafungamano ya tamaa za kinafsi. Basi, njia za yakini hii iliyokamilika haziwezi kamwe kufunguka kwa mipango ya kibinadamu. Na falsafa zilizobuniwa za kibinadamu hapa hazileti faida yoyote, bali daima Mwenyezi Mungu huteremsha nuru hii kutoka mbinguni katika wakati wa giza, kwa kupitia waja wake makhsus. Na ateremkaye toka mbinguni ndiye apelekaye huko mbinguni.

Basi enyi watu mlio fukiwa ndani ya shimo lenye kiza, na mliokamatwa na makucha ya dhana na shaka, na mlio watumwa wa tamaa za nafsi, msiringie Uislamu wa jina tu na wa dhahiri, na msiifahamu mipango hii inyofanywa na vyama na madarasa za siku hizi kuwa ndizo zenye kuwaleteeni ustawi na maendeleo ya kweli na mafanikio yenu ya mwisho. Shughuli hizo kimsingi zinatafaa na zinaweza kufikiriwa kuwa ni kipago cha kwanza cha maendeleo, lakini ziko mbali sana na shabaha ya kweli. Labda kutokana na mipango hiyo uzalike ujanja wa akili au mwelekeo wa kiuayari na ukali wa kiubongo, na mazoezi ya mantiki kavu yapatikane, au inyakuliwe lakabu ya ushehe na uanazuoni; na pengine baada ya muda mrefu kupata elimu yawezekana pia wawe wasaidizi kidogo kwa maksudio yenye. Lakini (wasemavyo waajemi) kabla ya kuwasili tiba toka Iraki, aliyeumwa na nyoka atakuwa ameisha kufa tayari.

Basi amkeni na zindukeni, isije mkajikwaa, isije safari ya akhera ikakukuteni katika hali ya ukafiri na upotevu. Fahamuni kwa yakini kwamba mategemeo yote ya matumaini ya kufaulu katika akhera hayawezi kuwa kupata elemu hizi za kawaida. Na iko haja ya kuteremka nuru ya kimbunguni ambayo huziondolea mbali takataka za shaka na wasiwasi na kuzima moto wa tamaa za nafsi na kuvutia kwenye upendo wa kweli na akili ya kweli na utii wa kweli wa Mwenyezi Mungu. Kama mkiuliza dhamiri yenu, mtajibiwa kwamba ule utulivu wa kweli ambao mara moja husababisha mabadiliko ya kiroho, hamjaupata bado hadi sasa. Basi ni

masikitiko makubwa kabisa kwamba hamjali silsila ya kimbunguni hata sawa na sehemu ya mia kuliko jazba mliyo nayo ya kueneza mambo na elimu za kawaida. Maisha yenu yanatolewa wakfu zaidi kwa mambo ambayo kwanza hayana uhusiano wowote wa dini, na kama unao basi uhusiano huo ni wa daraja la chini kabisa ulio mbali sana na shabaha ya asili. Kama mkiwa na hisia na akili inayofikia shabaha ya lazima, basi kamwe hamwezi kutulia mpaka mjipatie shabaha hiyo ya asili. Enyi watu! Nyinyi mmeumbwa kwa kumtambua na kumpenda na kumtii Mungu wenu wa kweli, Mwumba wenu wa asili na Mwabudiwa wenu hasa.

Basi maadamu jambo hili ambalo ndilo shabaha hasa ya kuumbwa kwenu halijadhihirika kwa uwazi ndani mwenu, mko mbali sana na wokovu wenu wa kweli. Mkisema kwa uadilifu, nyinyi wenyewe mnaweza kuwa mashahidi wa hali yenu ya ndani kwamba, badala ya ibada ya Mwenyezi Mungu, kila wakati, mbele ya moyo wenu, kuna sanamu kubwa kabisa la ibada ya dunia, ambalo kila sekunde mnalisujudia mara elfu kadhaa na nyakati zenu zote zenyet thamani zinapotea katika porojo za kidunia hata kwamba hamna fursa ya kutazama upande mwingine. Je, mmekumbuka wakati wowote kuwa mwisho wa maisha haya ni nini? U wapi uadilifu ndani yenu? I wapi amana ndani yenu? U wapi ukweli ndani yenu na ucha-Mungu na uaminifu na unyenyekevu ambao kwao Kurani inakuiteni? Kwa miaka na miaka hamkumbuki hata kwa bahati kwamba tunaye Mungu pia. Haipiti moyoni mwenu mnazo haki zake zifi juu yenu. Ukweli ndio huu

tu kwamba nyinyi hamna uhusiano wowote, mwungano wowote na fungamano lolote na yule Qayumu¹⁶ wa kweli na inakuwa shida kwenu hata kulitaja jina lake. Sasa kwa ujanja mtashindana kwamba si hivyo hata kidogo. Lakini kanuni ya maumbile ya Mwenyezi Mungu inawafedhesheni ambapo inawakumbusheni kwamba ndani mwenu hamna alama za wenge imani. Ingawa sawa na fikira zenu na mawazo yenu ya kidunia mnajidaia kwa nguvu busara na rai imara, lakini umahiri wenu na utambuzi wenu na busara zenu zinaishia duniani tu. Wala kwa akili yenu hii hamwezi kuona hata kona moja ya akhera ambayo roho zenu zimeumbwa kukaa humo milele. Nyinyi mmetulia kabisa na maisha ya dunia kama vile mtu anyetulia na kitu cha kudumu milele. Lakini ile akhera ambayo furaha zake ni zenyе kuleta utulivu wa kweli na ni za kudumu, hiyo hamwikumbuki hata mara moja katika maisha yote. Ni bahati mbaya ilioje kwamba mmeghafilika kabisa na jambo lililo kubwa na la muhimu, na mmekaa mkifumba macho kabisa, na katika tamaa ya yale mambo ya kupitapita tu mnakimbia sana huko na huko usiku na mchana. Mnatambua sana kwamba bila shaka wakati ule unakujieni ambao mara moja utayamaliza maisha yenu na matarajio yenu. Lakini hii ni bahati mbaya ya ajabu kwamba juu ya kufahamu haya bado mnaziangamiza nyakati zenu zote katika kuitaka dunia. Na kuitaka dunia hukuishia tu kwenye njia zinazojuzu, bali mmekwisha halalisha njia zote zisizojuzu kuanzia uwongo

¹⁶ Hili ni jina la Mwenyezi Mungu. Maana yake ni yule ambaye anajitegemea na wote wanamtegemea ye. (mwenezi)

na ulaghai hadi kumwaga damu pasipo haki. Na pamoja na uhalifu wote huo wenye kufedhehesha ulioenea kati yenu, mnasema kwamba hatuhitaji nuru wala silsila yoyote ya mbinguni, bali mnaifanyia uadui mkubwa kabisa. Nyinyi mmeiona silsila ya Mwenyezi Mungu ya kimbungunui hafifu kabisa hata kwamba kwa kuitaja ndimi zenu zinaikashifu kabisa kwa maneno yaliyojaa chuki katika hali ya kiburi na kubeua. Nanyi mnasema mara kwa mara tutakuwaje na yakini kwamba silsila hii imetoka kwa Mwenyezi Mungu. Nimeshatoa jibu lake sasa hivi kwamba mtatambua mti huu kwa matunda yake, na juu hili kwa mwanga wake. Nimekwisha wafikishieni ujumbe huu mara moja, sasa ni hiyari yenu kuukubali au kuukataa, na kuyakumbuka maneno yangu au kuyasahau kabisa.

Mtu hathaminiwi maadamu yuko hai, enyi wapenzi. Maneno yangu mtayakumbuka baada yangu.

Mwisho: Shairi la Kucombezea kuvurugika hali ya Islamu

[Tafsiri ya Shairi la Kiajemi]

Yafaa jicho la kila Mwislamu litokwe machozi kwa uchungu juu ya hali mbaya ya Islam na Waislamu wa kweli kukosekana.

Dini ya haki imefikiwa na wakati mgumu na wenye kutisha. Uchafuzi umetapaka duniani kwa sababu ya kufuru na inadi.

Yule ambaye nafsi yake haina kheri wala uzuri, naye anamtolea aibu nyingi yule aliye mbora wa Mitume.

Na yule aliyefungwa mwenyewe ndani ya jela ya unajisi, pia anapiga domo kuhusu shani ya imamu wa watukufu.

Habithi mwovu amrushia mishale aliye maasumu. Yafaa mbingu ivurumishe mawe katika ardhi.

Mbele ya macho yenu Islam imeanguka katika vumbi; mna udhuru gani mbele ya Mwenyezi Mungu, enyi kundi la matajiri!

Kila upande kufuru inafura kwa kishindo kama majeshi ya Yazidi. Dini ya haki ni mgonjwa na bila msaada kama Zainul Abidiin.

Watu wenye uwezo wamejitosa katika maisha yao ya anasa wakibarizi na wanaweke warembo kwa vicheko na furaha.

Masheikh wa dini, usiku na mchana wanagombana kwa hasira ya nafsi. Na watawa wameghafilika kabisa na mahitaji ya dini.

Kila mmoja amejichagulia upande mmoja kwa nafsi yake duni, na upande wa dini u mtupu na kila adui ameruka kutoka maoteo.

Enyi Waislamu, je, hizi ndizi alama za Kiisalamu! Dini ina hali mbaya, nanyi mmeushikilia mzoga wa dunia.

Jumba la dunia li imara kiasi gani machoni mwenu! Ama pengine mmekwisha sahau habari za mauti ya waliotangulia.

Wakati wa mauti umekaribia, enyi mlioghafilika; yazingatieni. Kikao cha kileo pamoja na vipusa wazuri na warembo kitaendelea mpaka lini?

Ewe mwenye akili, usijifungie nafsi yako na dunia, au la utaona uchungu mwingi wakati wa kukata roho.

Usimpende yejote kwa moyo ila Yule Mpenzi Ambaye uzuri Wake ni wa milele, ili upate furaha ya kudumu kutoka kwa Mbora wa wafanyao hisani.

Mwenye akili ndiye yule asiyejali kitu katika njia Yake; na azindukaye ndiye aliyejilevyta kuona uso wa Mpenzi Huyo Mzuri.

Kikombe cha ashiki yake ni maji ya uhai wa milele; akunywaye hicho hatakufa kamwe.

Ee ndugu! Usiingiwe na mapenzi ya mali ya dunia iliyodhalili, kuna sumu iangamizayo katika kila tone la asali.

Ujitalidi kadiri uwezavyo kwa ajili ya dini, kwa uhai na mali, ili upate toka kwa Mola wa Arshi tuzo ya kushangiliwa mara mia.

Kwa amali hakikisha ile nuru iliyomo ndani ya imani yako; kama umekwisha ingiwa na huba ya Yusufu, basi na ishike njia ya Kanani.

Twakumbuka siku ambapo dini iliendewa na watu wa kila dini, nayo ikawaachisha huru katika njia ya Shetani mlaaniwa.

Ilieneza kivuli cha ulezi bora kwa nuru ya elimu duniani kote, na mguu wake ulikuwa juu mbinguni kwa sababu ya staha na heshima.

Zimewadia sasa zama ambapo kila mpumbavu punguani anakadhibisha kwa ujinga dini hii madhubuti.

Malaki ya wapumbavu wemetoka katika dini, na malaki ya wajinga wakawa windo la wenye hila.

Waislamu wamepata pigo la dhila yote kwa sababu kuhusu dini hima yao haikulingana na ghera yao.

Hata kama ulimwengu ukiritadi dini ya Mustafa s.w.a, hawatikisiki kwa ghera hata sawa na kiinitete.

Fikara yao saa zote huhangaikia dunia hii dhalili na mali yao huangamia katika njia ya wake na watoto wao.

Hao katika kikao chochote cha upujufu huwa vinara. Nao ndio vito popote palipo mahafili ya maasi.

Wanayajua sana mabaa, lakini hawaujui mtaa wa mwongozo, wanawachukia viongozi wa dini na wanajikalia pamoja na walevi.

Yule Mpandwa Aliyekuwa na ikhlasi tele Aliwapa kisogo Asipoona miyoni mwa kaumu hii ukweli wa waliohalisika.

Zama zile za dola na sudi yao njema zimepita tayari.
Nuksi ya amali zao imewaletea hizi siku.

Kwa njia ya kutumikia dini maendeleo ya hali ya
juu yalipatikana awali; yakipatikana tena, bila shaka
yatakuwa kwa njia iyo hiyo.

Ee Mwaabudiwa wangu, wakati wa msaada kutoka
kwako utawadia lini, na lini tutaona tena zile siku na
miaka ya baraka?

Fikra hizi mbili kuhusu dini ya Ahmad s.a.w. zimeyeyusha
kiini cha uhai wangu: wingi wa maadui na uchache wa
wasaidizi wa dini.

Ee Mungu, njoo haraka na tunyeshee mvua ya misaada
yako au la niondoe toka mahali hapa penye moto.

Ee Mungu, lete mwanga wa mwongozo toka chanzo
cha rehema; yaangazie macho ya waliopotea kwa ishara
zilizo wazi.

Kwa kuwa umenijaalia ukweli katika uchungu na
majonzi, siwezi kutarajia kwamba Utanifisha katika hali
ya kushindwa katika habari hii.

Kazi ya wakweli haibaki bila kukamilika; kwa wakweli,
mkono wa Mungu hufichikana mkononi mwa vazi lao.

TANGAZO KWA WAPENZANI WOTE

Tumedhamiria kwamba katika zama hizi madhehebu mbalimbali na watu wa rai tofauti wanaopinga Uislamu au mafundisho ya Kurani au kumpinga Seyyid na Bwana wetu Mtukufu Mtume wa Mungu s.a.w. au wanaotutafutia makosa katika mambo yetu au walio na shaka na wasiwasi kuhusu funuo zetu na madai yetu yanayolingana na funuo zetu, tuorodheshe makinzani hayo yote na kuchapa kwa sura ya kijitabu na kuanza kujibu kila ukinzani na swali moja baada ya jingine. Hivyo, wanatangaziwa wote kwa jumla, Wakristo, Mabaniani, Waaria, Wayahudi, Majusi, Madahariyya, Wabrahmu, Wanasyansi, Wanafalsafa, na Waislamu wenye rai tofauti n.k. kwamba kila mtu aliye na upinzani kadhaa dhidi ya Islamu au Kurani Tukufu au Seyyidna Mwongozi wetu, Mbora wa Mitume au dhidi yetu au dhidi ya cheo chetu tulichojaaliwa na Mwenyezi Mungu au dhidi ya funuo zetu, basi kama yu mtafuta ukweli analazimika na kuwajibika kwamba atuletee upinzani huo wote kwa kuandika kwa maandishi safi ili upinzani huo wote ukusanywe mahali pamoja na kuorodheshwa na kupangwa na kupigwa chapa katika kijitabu kimoja, na kisha kila upinzani ujibiwe kirefu, mmoja baada ya mwingine. [وَالسَّلَامُ عَلَى مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَىٰ. *[Salamu iwe juu ya afuataye mwongozo]*]

Mtangazaji, Mnyenyeketu:
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,
Wilaya ya Gurdaspur, Panjab. 10 Jamada II 1308 Hijria.

TANGAZO

Pamoja na kijitabu hiki vijitabu vingine viwili vimetungwa, ambavyo kwa hakika ni sehemu za kijitabu hiki. Kijitabu hiki chaitwa *Fat'he Islam* na cha pili *Taudhihe Maram* na cha tatu *Izalah Auham*.

Mtangazaji
Mirza Ghulam Ahmad
Kutoka Qadian.